# KIONGOZI CHA

# SHERIA

Hakimiliki© 2008

Kimetolewa na:
**Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC)**

Waandishi: wa Toleo la 5

Scholastica Jullu
Athanasia A. Soka
Safina Hassan
Mary Njau

Toleo la 5: 2008

ISBN 978–9987–22–056–4

Kimefadhiliwa Na:
Friedrich-Ebert-Stiftung, Dar es Salaam, 2008

# DOKEZO

Kiongozi hiki cha Sheria kimeandaliwa na wajumbe wa kujitolea wa Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake, (WLAC) kwa ajili ya Wasaidizi wa Sheria ambao si wanasheria (Paralegals) ambao wana moyo wa kuwasaidia wanawake na watoto. Friedrich-Ebert-Stiftung wamefadhili uandishi na uchapaji wa Kiongozi hiki, kwa matarajio kuwa kitasaidia kuinua hali ya wanawake wa Tanzania kwa kuongeza ufahamu wa sheria na haki zao. Tunatumaini kuwa Kiongozi hiki kitaweza kufanikisha madhumuni hayo ambapo itasaidia katika nyanja zote za maendeleo.

This edition of “Kiongozi cha Sheria” was prepared by volunteering members of the Women’s Legal Aid Center (WLAC) in order to assist members of Paralegal Units and the public at large, who have an interest in promoting women’s and children’s rights in Tanzania. The Friedrich-Ebert-Stiftung continues to support the compilation and printing of the “Kiongozi cha Sheria” hoping that it will help raising Tanzanian women’s legal conditions through deepening their awareness of different existing laws and their legal rights. It is hoped that the “Kiongozi cha Sheria” will fulfill this intention and will be helpful in different contexts of gender development.

# SHUKRANI

Kiongozi hiki cha sheria kinalenga kuelimisha jamii juu ya sheria mbalimbali zinazomgusa mwanamke na mtoto na haki zao. Ni nyezo ya kutumiwa na wasaidizi wa sheria (paralegals) na hata mashirika mbalimbali kufundishia jamii, ukizingatia uelewa wa watu kuhusu sheria hususani zinazogusa haki za wanawake ni mdogo. Kiongozi hiki tangu toleo la kwanza kimeendelea kuwa cha manufaa makubwa katika kuelimisha jamii.

Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC) kinapenda kutoa shukrani zake za dhati kwa wanasheria wa kujitolea katika shirika hili kwa kuandaa toleo la kwanza la kitabu hiki ambao ni: Dr. Monica E. Mhoja, Bibi Lucy P.Nambuo, Bwana Evod H. Mmanda, Bibi Helen Kijo-Bisimba na Bibi Scholastica Jullu.

Shukrani za pekee zimwendee mfadhili wa kiongozi hiki Friedrick-Ebert-Stifing (FES) kwa kufadhili uandishi na uchapaji wa kiongozi hiki kuanzia toleo la kwanza.

# YALIYOMO

**UKURASA**

DOKEZO.............................................................................i
SHUKRANI ........................................................................ii
UTANGULIZI...................................................................... v

**SURA YA KWANZA**
**SHERIA YA ARDHI**............................................................ 1
Sheria ya Ardhi ya Vijiji 1999.............................................. 13
Nafasi ya Mwanamke katika kumiliki Ardhi ya Kijijij................. 14
Usuluhishi, utatuzi wa Migogoro na uwakilishi wa wanawake
Katika vyombo vya utatuzi wa migogoro ya Ardhi.................... 20

**SURA YA PILI**
**SHERIA YA NDOA**.............................................................. 25
Maana ya Ndoa.................................................................... 27
Aina za Ufungaji wa Ndoa na Taratibu za Kufuata.....................31
Ndoa Batilifu na sababu zinazoweza kuifanya
Ndoa kuwa Batilifu.............................................................. 35
Haki na wajibu katika Ndoa.................................................. 39

**SURA YA TATU**
**TALAKA**........................................................................... 44
Maana ya Talaka.................................................................. 45
Sababu za kutoa Talaka........................................................46
Taratibu za kufuata wakati wa Kuvunja Ndoa........................... 49
Mifano ya Maamuzi ya Kesi za Talaka...................................... 50

**SURA YA NNE**
**HAKI ZA MTOTO** ........................................................................ 54
Haki za Mtoto Kimataifa............................................................. 57
Haki za Mtoto Tanzania............................................................ 61

**SURA YA TANO**
**SHERIA ZA MIRATHI**................................................................ 78
Utangulizi.................................................................................... 79
Sheria zinazotumika katika masuala ya Mirathi Tanzania....... 80
Mifano ya Maamuzi ya Kesi za Mirathi........................................ 89
Wosia.......................................................................................... 91
Taratibu za kufungua Mirathi...................................................... 95
(i) Wosia ukiwepo........................................................................ 95
(ii) Kama hakuna Wosia.............................................................. 95

Mfano wa wosia.......................................................................... 98

**SURA YA SITA**

**SHERIA YA MAKOSA YA KUJAMIIANA**...................................... 100
Utangulizi.................................................................................... 101
Mabadiliko katika Sheria zinazogusa Makosa ya Kujamiiana... 102
Kosa la Kubaka........................................................................... 104
Ukatili kwa watoto...................................................................... 112
Adhabu la Kosa la ukatili kwa watoto........................................ 112

**SUMMARY IN ENGLISH**............................................................ 120
**GLOSSARY**............................................................................... 144

# UTANGULIZI

## UTANGULIZI

Kukua na kupanuka kwa jamii yetu kumekwenda pamoja na kupanuka kwa mahusiano ya watu katika jamii. Ili mahusiano haya yakue na kuendeleza jamii, imekuwepo haja ya kuwa na kanuni na taratibu za kisheria ili kuongoza na kuboresha haya mahusiano. Pale inapotokea kwamba hakuna sheria ya kuongoza jambo Fulani, au sheria ipo lakini inatafsiriwa vinginevyo au haieleweki na walengwa waliokusudiwa, hatima yake ni kutokea kwa misuguano au manung'uniko.

Nchini Tanzania katika miaka ya hivi karibuni, limekuwepo shinikizo toka sehemu mbalimbali za makundi tofauti yanayotetea haki za akina mama la kuitaka jamii nzima ya Watanzania kuangalia upya suala la hadhi ya mwanamke katika jamii. Mwelekeo huu mpya umetokana na upungufu ulijitokeza katika sheria mbalimbali, matumizi ya baadhi ya mila na desturi katika jamii na kwa ujumla maendeleo makubwa ambayo baadhi ya akina mama wamepata pamoja na nafasi ya uongozi katika nyanja za elimu, uchumi, siasa n.k.

Pamoja na nia hii ya kutoa msukumo ili kuchochea mabadiliko na marekebisho ya sheria na mila zilizopitwa na wakati imeonekana kuna haja ya wale wote ambao wameamua kujihusisha na kutetea haki za wanawake kuwa na uelewa kuhusu tatizo lenyewe na mbinu za kufanikisha nia hiyo. Hapa tuna maana ya kuwa, wanapaswa kujua sheria zinasemaje, zina upungufu gani na nini cha kurekebisha, au kama hakuna sheria iliyokwishatungwa nini kifanyike ili sheria hiyo itungwe na kutekelezwa.

Kwa ajili hiyo basi Kiongozi hiki cha sheria, lengo lake kuu ni kutoa mwanga wa sheria

zinazomgusa mwanamke na mtoto moja kwa moja. Kiongozi hiki kitakuwa ni mwongozo kwa wale ambao wako mstari wa mbele katika kutetea haki za wanawake. Kitakuwa ni kiongozi cha kufundishia pale elimu ya aina hii itakapohitajika kwa wale ambao katika harakati hizi za kumkomboa mwanamke walikuwa hawajajihusisha. Kiongozi hiki kitachochea hisia na udadisi na hatimaye ushiriki wa kikamilifu katika harakati hizi. Kiongozi hiki kimegawanyika katika sura tano:

Sura ya Kwanza ya Kiongozi hiki inahusu Sheria za Ardhi. Sehemu hii inaangalia Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya kijiji. Ndani ya sheria hizi misingi Mikuu ya ardhi imeainishwa, usimamizi wa ardhi na umiliki wa ardhi yamefafanuliwa kwa ufasaha. Vilevile sura hii inazungumzia nafasi ya mwanamke katika kumiliki ardhi ya kijiji, utatuzi wa migogoro ya ardhi na makosa ya jinai yaliyoainishwa na sheria hizi.

Sura ya Pili inaelezea kuhusu Sheria ya Ndoa. sura hii inachambua nini maana ya ndoa, ni mambo gani muhimu kuyatimiza kabla ya kufunga ndoa, aina za ndoa, namna ya kugeuza ndoa, dhana ya ndoa na masharti yake. Mwisho inafafanua haki na wajibu wa wanandoa.

Sura ya Tatu ya Kiongozi hiki inaelezea Sheria inayohusu Talaka. Ndani ya sura hii inaelezwa talaka ni nini, sababu ya kutoa talaka na sababu zinazosababisha ndoa kuvunjika kutolewa kwa talaka. Mwisho imefafanua taratibu za kufuata kisheria ili talaka iweze kutolewa.

Sura ya Nne ya Kiongozi hiki inachambua kwa kina Haki za Mtoto. Inafafanua mtoto ni nani, hadhi mbalimbali anazopewa mtoto kisheria, haki za mtoto kimataifa, Mkataba

wa kimataifa wa Haki za mtoto. Pia inaelezea ni nani mwenye wajibu wa kumtunza mtoto. Ndani ya sura hii wajibu wa wazazi, jamii na taifa unafafanuliwa.

Sura ya Tano ya Kiongozi hiki inahusu Sheria ya Mirathi. Katika sehemu hii imefafanuliwa maana ya mirathi, Sheria zinazoshughulikia mirathi nchini Tanzania na namna sheria hizo zilivyoweka mgawanyo wa mali zilizoachwa na marehemu miongoni mwa warithi. Vilevile wosia umefafanuliwa – maana yake, aina za wosia na taratibu za kuandika wosia. Pia taratibu za kufuata katika kufungua mirathi kama kuna wosia au hakuna wosia, zimefafanuliwa.

Sura ya Sita na ya mwisho ya Kiongozi hiki inahusu Sheria ya Makosa ya Kujamiiana. Sura hii inaangalia mabadiliko katika sheria mbalimbali zinazogusa makosa ya kujamiiana.

Ni matumaini yetu kuwa wale wote watakaosoma kiongozi hiki watanufaika vya kutosha na elimu watakayoipata.

# SURA YA KWANZA

# SHERIA YA ARDHI

# UTANGULIZI

## Maana ya Ardhi

Ardhi inajumuisha tabaka la juu la nchi, vitu vilivyoota juu yake (mfano mimea na majengo), pamoja na vitu vilivyoko chini yake, isipokuwa madini na mafuta.

Ardhi ina umuhimu mkubwa katika maisha ya binadamu. Ardhi ni moja ya rasilimali ya msingi katika uhai na maendeleo ya binadamu, wanyama, mimea na viumbe vyote.

Katika uchumi unaotegemea kilimo kama sekta muhimu kukidhi mahitaji ya wananchi walio wengi, kama ilivyo hapa Tanzania, ardhi ni rasilimali muhimu ambayo kila mwananchi hana budi kuipata, kuimiliki, kuitumia na kuitunza. Aidha, ardhi ni rasilimali inayohitajika ili kuendeleza sekta nyingine za uchumi, zikiwemo viwanda, biashara na makazi ya binadamu ambayo hutegemea ardhi kwa ujenzi wa nyumba, barabara, kilimo na matumizi mengineyo. Hivyo basi, ardhi ni hitaji muhimu na pia ni haki ya kila binadamu na kumnyima mtu yeyote haki ya kumiliki, kutunza na kuitumia ni uvunjaji wa haki za binadamu.

Kwa muda mrefu sasa mila na desturi nyingi katika nchi yetu zimekuwa zikimnyima mwanamke haki nyingi za msingi ikiwemo haki ya kumiliki ardhi, ukilinganisha na mwanaume. Ni baada ya kubaini ukweli huo na kutambua mchango wa mwanamke katika jamii ndio maana mambo mengi yanarekebishwa ili kuondoa tofauti zilizopo kati ya jinsi ya kike na ile ya kiume hususani katika haki za msingi walizonazo.

***Ni muhimu kuelewa kwamba, kwa muda mrefu sana, tangu***

***kipindi cha ukoloni na hata baada ya uhuru Tanzania ilikuwa inatumia sheria ya Ardhi ya 1923 ambayo haikuweka bayana suala la umiliki na matumizi ya ardhi ya vijiji zaidi ya sheria za mila, mpaka ilipopitishwa Sheria ya Ardhi ya Kijiji mwaka 1999.***

Hivyo, Sheria za Ardhi za mwaka 1999 zimetungwa ili kuweka bayana masuala hayo na hususani kuondoa tofauti zilizopo katika kufanya maamuzi yanayohusiana na masuala ya ardhi.

**MGAWANYO WA ARDHI**

Sheria ya Ardhi 1999, Sura ya 113 Kama sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002 imeigawa ardhi katika makundi matatu, ambayo ni:

**(a) Ardhi ya jumla**

Hii ni ardhi ambayo, siyo ya kijiji wala hifadhi.

**(b) Ardhi ya Kijiji**

Ardhi hii imeelezwa Kwa kina chini ya Sheria ya Ardhi ya Kijiji Sura ya 114 kama sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002. Hii ni ardhi iliyo ndani ya mipaka ya kijiji na ambayo imesajiliwa kwa kufuata sheria zilizowekwa.

**(c) Ardhi ya Hifadhi**

Hii ni ardhi ambayo imetengwa kwa madhumuni maalumu nayo ni pamoja na:

- Maeneo ya hifadhi ya misitu,
- Mbuga za wanyama pori,
- Hifadhi za maji (bahari, mito, mabwawa, maziwa n.k),
- Ardhi yenye majimaji,
- Hifadhi ya barabara,
- Maeneo ya wazi,
- Maeneo yaliotangazwa kuwa ni ardhi ya hatari n.k.

**MUHIMU**

Sheria hizi zimezingatia msingi wa usawa na haki katika kumiliki ardhi. Sheria zimeeleza bayana kuwa, haki ya kila mwanamke kupata, kumiliki, kutumia na kushugulikia masuala yanayohusu ardhi, itakuwa sawa na kwa masharti yaleyale kama ilivyo kwa mwanaume.

Sheria imeondoa ubaguzi dhidi ya wanawake. Hivyo mwanamke anayetaka ardhi, atafuata taratibu zote zinazohusika, na hapaswi kunyimwa ardhi kwa sababu tu yeye ni mwanamke.

**SHERIA YA ARDHI NA. 4 ya 1999**

Sheria hii inazungumzia masuala ya usimamizi wa ardhi, umilikaji, uwekaji rehani, upangaji, utatuzi wa migogoro ya ardhi, pamoja na mambo yanayohusiana na ardhi kwa ujumla.

Ni muhimu kuelewa kwamba, ardhi inayozungumziwa katika sheria hii, haihusiani na ardhi ya kijiji kwa sababu usimamizi wa ardhi ya vijijini na masuala yote yanayohusiana nayo yanashughulikiwa na Sheria ya Ardhi ya kijiji No. 5 ya mwaka 1999.

**Usimamizi wa ardhi**

Kwa mujibu wa sheria za ardhi, zipo ngazi mbalimbali za usimamizi na utekelezaji wa masuala ya ardhi kama ifuatavyo:

**i. Rais**

Ndiye msimamizi mkuu wa masuala yote ya ardhi Tanzania. Ana wajibu wa kumteua Waziri wa Ardhi na Kamishna wa Ardhi. Ana uwezo wa kubadilisha ardhi kutoka kundi moja kwenda jingine (mfano ardhi ya kijiji kuwa hifadhi au kinyume chake)

**ii. Waziri wa Ardhi**

Wajibu wake mkuu ni kuunda Sera ya Ardhi ya Taifa na

kusimamia utekelezaji wa sera hiyo. Pia anatakiwa kusimamia utekelezaji wa Sheria za Ardhi na ana uwezo wa kuunda kamati za kugawa ardhi na baraza la taifa la ushauri la ardhi.

**iii. Kamishna wa Ardhi**

Ndiye mtendaji na mshauri mkuu wa masuala ya ardhi Tanzania. Anawajibika kutoa nyaraka, miongozo na maelekezo mbalimbali juu ya utekelezaji wa sera na Sheria za Ardhi. Anawajibika pia kutayarisha ripoti ya mwaka juu ya utendaji mzima wa masuala ya ardhi.

**iv. Kamati za ugawaji wa ardhi**

Humshauri na kumsaidia Kamishna wa Ardhi kuhusu maombi ya kumiliki ardhi katika sehemu za makao makuu, mijini na wilayani.

**v. Baraza la Taifa la ushauri la ardhi**

Huangalia na kupitia upya masuala ya ardhi na muundo wa kazi na kumshauri waziri juu ya sera ya Taifa ya ardhi kwa nia ya kutoa mapendekezo na kufanya mabadiliko inapobidi.

**vi. Halmashauri ya wilaya**

Hutoa ushauri na mwongozo kwa kila Halmashauri ya kijiji iliyoko kwenye eneo la Halmashauri hiyo, juu ya usimamizi na uendeshaji wa kazi zake. Hata hivyo ushauri na miongozo hiyo haitakiwi kutofautiana au kwenda kinyume na nyaraka au maelezo ya kamishna wa ardhi.

**vii. Halmashauri ya kijiji**

Inawajibika katika masuala yote ya usimamizi, ugawaji na utunzaji wa mipaka ya ardhi ya kijiji kwa kufuata ushauri na miongozo inayotolewa na uongozi uliopo juu yake. Ina uwezo wa kuunda kamati ya maamuzi ya kijiji na kutoa

ushauri, mwongozo na mapendekezo kwa kamati hiyo juu ya utekelezaji wa kazi zake.

**viii. Mkutano mkuu wa kijiji**

- Hupitisha maombi ya umiliki wa ardhi kijijini.
- Hutoa ushauri na mwongozo wa utendaji kwa halmashauri ya kijiji.

**ix. Kamati ya maamuzi ya kijiji**

- Hutambua ardhi ya kijiji na mipaka yake.
- Hutenga au kuweka akiba ya ardhi au kutoa mipaka ya haki ya njia na haki zingine za kutumia njia ambazo itaziona ni muhimu kwa umiliki bora wa ardhi.
- Hulinda maslahi ya wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wanakijiji wasiokuwepo kijijini.

Sheria hii imempa Waziri anayehusika na ardhi uwezo wa kuunda "KAMATI ZA UGAWAJI ARDHI" katika ngazi za uongozi wa serikali za makao makuu, mijini na wilayani. Kamati hizi zitakuwa na jukumu la kumshauri kamishna wa ardhi kuhusu maombi ya kumiliki ardhi.

Waziri pia amepewa mamlaka ya kuunda BARAZA LA KITAIFA LA USHAURI WA ARDHI ambalo linatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua saba (7) na wasiozidi kumi na moja (11). Mwenyekiti wa baraza hilo atachaguliwa na Rais. Sheria hii inamtaka waziri, kuhakikisha kuwepo kwa uwiano sawa baina ya wanawake na wanaume wakati wa kuunda kamati za ugawaji wa ardhi.

**Nani anaweza kuomba haki ya kumiliki ardhi chini ya Sheria ya Ardhi?**

Chini ya sheria ya ardhi mtu au watu wanaoweza kuomba haki ya umiliki wa ardhi ni:-

- Mwanamke au mwanaume Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

- Kikundi cha watu wawili au zaidi ambao ni raia wa Tanzania na ambao wamejiunga pamoja chini ya sheria hii au sheria zingine za Tanzania.
- Mtu yeyote au kikundi chochote cha watu ambao ni raia au si raia wa Tanzania wanaweza kuomba umiliki wa ardhi, lakini watapata haki miliki isiyo asili (derivative rights) kwa ajili ya uwekezaji).
- Mtu ambaye si raia wa Tanzania hawezi kupewa haki ya kumiliki ardhi isipokuwa kwa madhumuni ya uwekezaji chini ya Sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997.

**Umiliki wa ardhi chini ya sheria ya Ardhi**

Kuna aina mbili za umiliki wa ardhi, nazo ni:

i. Umiliki wa mtu binafsi: sheria inatoa nafasi na haki kwa mwanamke au mtu mwingine yeyote kuomba na kumiliki ardhi yake yeye binafsi, hata kama ameolewa.
ii. Umiliki wa pamoja (co-occupancy): Huu ni umiliki wa zaidi ya mtu mmoja.

Umiliki huu wa pamoja uko wa aina mbalimbali:-

i) Umiliki wa pamoja wa hisa zinazogawanyika (tenancy in common). Chini ya umiliki huu, endapo mmiliki mmoja atafariki basi hisa zake zitahamia kwa warithi wake.
ii) Umiliki wa pamoja wa hisa/maslahi isiyogawanyika (joint tenancy). Sheria imeweka bayana kuwa, umiliki wa aina hii unatolewa kwa idhini ya mahakama kuu tu. Chini ya umiliki huu, endapo mmiliki mmoja atafariki basi hisa zake zitahamia kwa wamiliki au mmiliki aliyebaki (right of survivorship). Hii ina maana ya kuwa warithi wake hawana haki ya kurithi bali wale wa mmiliki

wa mwisho atakayekuwa amebakia.

***Sheria imeweka bayana kwamba umiliki wa pamoja wa hisa zisizogwanyika utakaochukuliwa bila kibali cha mahakama ni ule wa mke na mume. Watu wengine wote watakaopenda kumiliki ardhi chini ya umiliki wa ardhi wa pamoja wa hisa isiyogawanyika watalazimika Kwanza kupata Kibali cha mahakama***

**MUHIMU**

Kila mmiliki wa pamoja atapewa hati yake ya umilikaji wa pamoja. Wanawake wahakikishe kuwa wanapata hati ya umilikaji. Pia, ugawaji wa ardhi inayomilikiwa kwa pamoja hauwezekani na haurususiwi, ila tu: -

- Iwapo wamiliki wote kwa pamoja, mfano mume na mke wataridhia kugawa ardhi hiyo.
- Iwapo mmiliki mmoja anaamua kuwapa au kutoa hisa zake kwa wale wamiliki wengine wa pamoja tu.

**Umiliki wa pamoja na mahusiano baina ya wanandoa**

- Mwanandoa mmoja anapoomba hati miliki ya ardhi atatakiwa kueleza bayana kama anachukua hati miliki hiyo kwa ajili yake binafsi au kwa ajili ya familia katika hati miliki ya pamoja kwa maslahi au hisa zisizogawanyika.
- Endapo jambo hili halitawekwa bayana, hati miliki itachukuliwa kuwa ya umiliki wa pamoja wa hisa zinazogawanyika.
- Inapotokea kwamba mwanandoa anamiliki ardhi au nyumba kwa jina lake mwenyewe na mwanandoa mwenzie amechangia nguvu zake katika kutunza au kuendeleza nyumba au

ardhi hiyo, mwanandoa aliyechangia ana haki pia.

**Taratibu za kuomba umiliki wa ardhi**

Sheria hii inaeleza taratibu zifuatazo**:**

1. Maombi yawekwe na kuwasilishwa kwenye fomu maalumu inayoambatanishwa na picha ya mwombaji.
2. Maombi hayo yawasilishwe wilayani au wizarani



***Wanawake na wanaume waha haki sawa ya kupata, kutumia na hata kugawa ardhi kwa kadri ya sheria zinavyoelezekeza***

1. Maombi yaambatanishwe na ada kama inavyoelezwa kwenye sheria.

2. Fomu isainiwe na mwombaji/mwakilishi au wakala wa mwombaji.
3. Maombi yaeleze au yaambatanishe taarifa inayotakiwa ambayo kamishna wa ardhi ataiomba kwa maandishi.
4. Maombi yaambatanishwe na orodha ya mali nyingine zinazohusiana na ardhi anayomiliki mwombaji kwa wakati huo.
5. Endapo sheria inataka idhini ya mamlaka ya serikali au mamlaka ya chombo chochote kabla ya kutoa idhini ya kumiliki ardhi ni vema kukamilisha hatua hii.
6. Kama ombi ni la mgeni au kampuni ya kigeni liambatanishwe na cheti cha kuidhinishwa na kitengo cha uwekezaji kwa mujibu wa sheria ya uwekezaji ya 1997.
7. Baada ya kupokea nyaraka na maelezo yote yanayohitajika, kamishna ataanza kushughulikia ombi kwa kufuata sheria inavyoagiza.

**Kugawa au kuhamisha haki ya kumiliki ardhi**

Sheria inaeleza kuwa mtu yeyote anayetaka kugawa haki yake ya kumiliki ardhi, anawajibika kutoa notisi kwa kujaza fomu na kuipeleka kwa kamishna au Afisa Ardhi anayehusika ili apate kibali cha kugawa au kuhamisha ardhi hiyo.

Sheria inaruhusu mtu kurejesha haki yake ya kumiliki ardhi kwa Kamishna wa ardhi. Hata hivyo Kamishna hatakubali kurejeshwa kwa ardhi yote au sehemu ya ardhi pale ambapo kurejeshwa kwa haki hiyo kunafanywa kwa

makusudi ya kumnyima mwanandoa (mwanamke) haki yake katika ardhi hiyo.

Kamishna hatakubali maombi ya kurejeshwa kwa ardhi hasa pale ambapo ardhi hiyo inamilikiwa na watu wawili au zaidi, na mmiliki mmojawapo hajakubali kurejeshwa kwa ardhi hiyo kwa maandishi. Pia pale ambapo mwanamke anamiliki ardhi pamoja na mume wake, hati ya maandishi kutoka kwa mwanamke inayoonesha kukubali kurejeshwa kwa ardhi hiyo itahitajika.

**MUHIMU:**

Mwanamke amepewa nafasi zaidi ya kumiliki ardhi pale ambapo mume wake atataka kurudisha ardhi. Kama mume ana mke zaidi ya mmoja ataulizwa mke mkubwa kwanza kama ataichukua na watafuata wengine kwa utaratibu wa nani aliolewa kwanza.

**Kuweka ardhi rehani**

Sheria za Ardhi zinampa haki mmiliki wa ardhi kuweka ardhi yake rehani. Hata hivyo kuweka rehani ardhi au nyumba inayomilikiwa na wanandoa ni lazima kwanza ipatikane ridhaa ya mwanandoa/wanandoa wote na kama ni nyumba ya kuishi au ardhi inayotumika, ni lazima wanaoishi au kuitumia ardhi hiyo watoe ridhaa. Hivyo, maombi ya rehani yanatakiwa yajazwe katika fomu maalum na lazima kuwekwa saini na mwanandoa/wanandoa wa mkopaji kuthibitisha kukubali rehani hiyo. Iwapo itabainika kwamba mwanandoa hakutoa idhini, rehani hiyo itakuwa batili.

- Ni wajibu wa mkopeshaji kuchukua hatua za makusudi za kuthibitisha kwamba mkopaji ana ndoa au la na kwamba anayetoa ridhaa ni mwanandoa halali wa mkopaji.
- Rehani ya kimila itafuata taratibu za kimila

zinazotumika katika eneo hilo. Hata hivyo lazima zizingatie haki za wahusika.

- Ardhi iliyowekwa rehani itakuwa ni dhamana tu na si uhamisho wa umiliki.
- Iwapo mkopaji atakiuka masharti ya mkataba wa rehani, au atashindwa kurejesha mkopo kwa muda unaotakiwa/uliokubaliwa, basi mkopeshaji ana wajibu wa kumpa mkopaji taarifa kwa maandishi ya kushindwa kulipa na nini anataka kukifanya.

Taarifa hiyo ni lazima ioneshe**:**

1. Kiasi kinachodaiwa.
2. Kwamba mkopeshaji ana stahili yake katika rehani
3. Baada ya siku 30 za kupokea notisi, mkopeshaji anaweza kuuza ardhi iliyowekwa rehani.

Endapo mkopaji atashindwa kurejesha fedha alizokopa, basi mkopeshaji anaweza:

1. Kuteua mtu wa kukusanya pato litokanalo na ardhi iliyowekwa rehani.
2. Kupangisha ardhi iliyowekwa rehani.
3. Kuishi katika ardhi iliyowekwa rehani.
4. Kuiuza ardhi iliyowekwa rehani. Iwapo ardhi iliyowekwa rehani ni ardhi ya kijiji na mkopeshaji akaamua kuiuza ardhi hiyo, ni lazima iuzwe kwa:
   - Mwanakijiji au kundi la wanakijiji.
   - Kwa halmashauri ya kijiji
   - Kwa mtu ambaye si mwanakijiji aliyeidhinishwa na Halmashauri ya kijiji.

Amri ya mahakama hutolewa pale mkopeshaji anapotaka kuuza mali zifuatazo:

- Nyumba ya kuishi.
- Ardhi kwa ajili ya kilimo.
- Ardhi kwa ajili ya ufugaji
- Pale ambapo kuitwaa ardhi kwa amani ni vigumu.

Mkopeshaji haruhusiwi kujiuzia ardhi au nyumba iliyowekwa dhamana. Hata hivyo, akitaka kujiuzia:

1. Lazima iwe kwa ruhusa ya mahakama.
2. Anunue kupitia mnada wa hadhara na awe na dau la juu kuliko wote

**Angalizo**

Iwapo yule anayetaka kugawa au kuweka rehani atadanganya kuwa mwanandoa mwenzake amekubali, basi kugawa huko, au kuweka rehani kutakuwa BATILIFU, kutegemeana na wanandoa au mwanandoa ambaye hakutoa ridhaa.

**Ukodishaji na upangishaji**

Sheria pia inaruhusu mtu kukodisha/kupangisha ardhi au majengo au kutoa ardhi kwa leseni kwa muda maalum. Iwapo yule aliyepanga ardhi au majengo hakutimiza masharti ya upangaji, yule mwenye ardhi yake, anaweza kumpa mpangaji notisi ya siku 30 na siku hizo zikiisha bila kurekebisha kasoro iliyojitokeza, basi mpangaji atapaswa kuhama katika nyumba hiyo.

## SHERIA YA ARDHI YA VIJIJI SURA 114 (Kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002)

Kwa jumla sheria hii imewekeka utaratibu mpya wa umilikaji ardhi vijijini kwa sababu hapo awali hapakuwepo na sheria iliyopitishwa na bunge inayoeleza waziwazi kusimamia ardhi iliyoko vijijini. Hii ni kutokana na umuhimu wa ardhi kama inavyoelezwa kwenye Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 kuwa ardhi yote ina thamani, iwe ya vijijini au mijini na iwe imeendelezwa au la.

**Ardhi ya kijiji ni ipi?**

Sheria hii imefafanua kwa kina masuala mbalimbali yanayohusu ardhi ya kijiji. Kwa mujibu wa sheria hii, ardhi ya kijiji ni:-

- Ardhi iliyo ndani ya mipaka ya vijiji vilivyosajiliwa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya ya mwaka 1982) Sura ya 287 kama Sheria zilivyorebishwa mwaka 2002, na vijiji vilivyohusishwa chini ya Sheria ya Makazi ya mwaka 1965.
- Ardhi ambayo imemilikiwa na wanakijiji kwa muda wa miaka 12 au zaidi kabla ya kuanza kutumika Sheria ya Ardhi ya 1999.
- Ardhi ambayo Rais ameibadilisha kutoka kuwa ardhi ya jumla au ya hifadhi na kuwa ardhi ya kijiji.

  Rais hufanya hivyo kwa kumwelekeza waziri anayehusika kutangaza na kuitaarifu Halmashauri ya kijiji.

**Mgawanyo wa ardhi ya kijiji**

Sheria ya ardhi ya vijiji imeigawa ardhi ya kijiji katika makundi matatu, nayo ni:

- Ardhi iliyokaliwa na kutumiwa na mtu, familia au kikundi cha watu kwa mujibu wa sheria za kimila.
- Ardhi ya pamoja ambayo Halmashauri ya kijiji itapendekeza kwa kupitia mkutano wa kijiji maeneo na makusudio ya maeneo hayo.
- Ardhi ya makazi au matumizi ya jumuiya ambayo inaweza kutolewa kwa njia ya mgawo na Halmashauri ya kijiji.

**Nafasi ya mwanamke katika kumiliki ardhi ya kijiji**

Sheria hii pia imewapa wanawake haki katika kumiliki ardhi kimila, haki ambayo hapo awali ilikuwa haipo na kama ilikuwepo basi ni katika baadhi ya mila na desturi ambazo tunaweza kusema ni nzuri japokuwa ni chache sana.

Katika kueleza ni jinsi gani na kwa kiwango gani mwanamke amepewa nafasi katika kumiliki ardhi ya kijiji, ni vizuri

kuangalia sehemu kuu tatu za sheria hii ambazo zinafafanua juu ya:

- Utumikaji wa misingi ya sera ya Taifa ya Ardhi.
- Utawala na usimamizi wa ardhi ya vijiji ikiwa ni pamoja na utoaji na usimamizi wa haki ya kumiliki ardhi kimila.
- Usuluhishi unaohusu ardhi na mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi vijijini

**Utumikaji wa sera ya Taifa ya Ardhi**

Katika kuhakikisha nafasi ya mwanamke kumiliki ardhi ya kijiji, Sheria inaeleza wazi kuwa haki ya kila mwanamke katika kupata, kutumia na kugawa ardhi itakuwa sawa na kwa masharti yale yale kama ilivyo haki ya mwanaume. Sheria hii inaonesha wazi kuwa hakutakuwa na tofauti yoyote katika haki juu ya masuala ya ardhi kwa jinsi zote.

**Utawala na Usimamizi wa ardhi ya kijiji**

**1. Halmashauri ya kijiji**

Chini ya Sheria hii, masuala ya usimamizi wa ardhi ya kijiji yamewekwa mikononi mwa Halmashauri ya kijiji ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa 1982. Halmashauri ya kijiji itafanya shughuli hiyo kama msimamizi wa wanakijiji ambao ndio wanufaishwa. Hivyo basi, wanawake lazima waelewe kwamba wanayo nafasi kubwa katika kusimamia ardhi ya vijiji vyao iwapo watakuwa wajumbe wa Baraza la Ardhi la kijiji.

**2. Mkutano Mkuu wa Kijiji**

Sheria hii inaeleza kuwa Halmashauri ya kijiji haiwezi kumpa au kumgawia mtu yeyote yule haki ya kumiliki ardhi kimila pasipo kupata kibali cha Mkutano Mkuu wa kijiji. Ni kwa mantiki hiyo basi, wanawake wanayo nafasi nzuri kwa kupitia Mkutano Mkuu wa kijiji ambao wanaweza

kusimamia utoaji wa hati za kumiliki ardhi kimila.

Hii inawawezesha kuhakikisha kuwa haki inatendeka wakati wa kugawa ardhi. Si hivyo tu, pia katika kila mkutano wa kawaida na Mkutano Mkuu wa kijiji, Halmashauri ya kijiji inatakiwa kutoa taarifa na kupokea maoni ya wanakijiji juu ya utawala na usimamizi wa ardhi ya kijiji.

### 3. Kamati ya Maamuzi ya kijiji

Sheria imeipa kamati hii wajibu wa kutambua ardhi ya kijiji na mipaka yake, kutenga na kuweka akiba ya ardhi na kutoa mipaka ya haki ya njia na haki zingine za kutumia njia ambazo itaziona ni muhimu kwa umiliki bora wa ardhi. Pia ina jukumu la kulinda maslahi ya wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wanakijiji wasiokuwepo kijijini.

**MUHIMU:**

- Katika usimamizi wa ardhi ya kijiji Sheria hii ndiyo itakayotumika katika umilikaji wa ardhi kimila na kwamba pale ambapo sheria hii haiko wazi au hakuna sheria nyingine iliyotungwa na Bunge inayohusu suala hilo, basi sheria ya mila itatumika.
- Sheria hii imeweka bayana kuwa sheria za kimila zitakazotumika ni lazima ziendane na misingi ya Sera ya Taifa ya Ardhi, misingi ya haki za binadamu pamoja na sheria nyingine za Bunge zisizo za kibaguzi.
- Sheria za kimila zitakuwa ni batili na hazitatumika wala kupewa uzito wowote na Halmashauri ya kijiji au Mkutano Mkuu wa kijiji iwapo zitakuwa zinamnyima mwanamke au mtoto au mtu yeyote mwenye maumbile tofauti, haki yake ya kisheria ya kupata, kumiliki au kutumia ardhi.

- Kipengele hiki kinamlinda mwanamke dhidi ya Sheria za kimila ambazo ni potofu na pia kinampa nafasi mwanamke kuweza kuhakikisha kuwa mila na desturi potofu zinazomnyima mwanamke haki ya kumiliki ardhi kimila zinaachwa na hata kutokomezwa kabisa.

**Nani anaweza kuomba umiliki wa ardhi kijijini?**

Kama ilivyoelezwa hapo awali sheria hii imeweka bayana kuwa:

(i) Mwanamke, au mwanaume, yeyote ambaye ni mwanakijiji mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea anaweza kuomba hati ya kumiliki ardhi ya kijiji.

(ii) Mtu yeyote yule au familia yoyote ile au hata kikundi chochote cha watu kinachotambulika chini ya sheria ya mila au ambacho kimejiunga kama chama cha Ushirika.

(iii) Mtu yeyote ambaye ameolewa na kuachika au ameondoka kijijini hapo kwa zaidi ya miaka miwili, na mwanandoa mwenzake alikuwa mwanakijiji kabla ya kufunga ndoa na wote ni raia wa Tanzania, anaweza kuomba haki ya kumiliki ardhi kijijini. Hii inaonyesha na kuweka wazi nafasi ya mwanamke kupata ardhi katika kijiji chake na hata katika kijiji ambacho mumewe alikuwa Mwanakijiji kabla ya ndoa yao.

(iv) Mtu yeyote au kikundi chochote cha watu ambao si raia wanaweza kuomba haki ya kumiliki ardhi ya kijiji, ila ni lazima wawe na wadhamini wasiopungua watano, ambao ni wanakijiji na waonyeshe nia ya kuanzisha makazi ya kudumu katika kijiji hicho ndani ya kipindi cha miezi miwili tangu wakubaliwe ombi lao.

Katika kuhakikisha kuwa mwanamke ana nafasi sawa

katika kupata ardhi, sheria hii imeeleza wazi kuwa katika kutolea maamuzi maombi yoyote ya haki ya kumiliki ardhi kimila, baraza la kijiji litafanya hivyo kwa kuzingatia usawa wa watu wote, kama vile kuyapa uamuzi sawa maombi toka kwa mwanamke au kikundi cha wanawake na yale yanayotoka kwa mwanaume au kikundi cha wanaume.

**MUHIMU:**
Sheria hii si kwamba inampa mwanamke nafasi sawa na mwanaume katika kupewa ardhi tu, bali pia inajaribu kumlinda dhidi ya ubaguzi wowote ambao unaweza kufanywa dhidi yake.

**Utaratibu wa kuomba umiliki wa ardhi ya kijiji**

Ardhi ya vijiji sasa ina hadhi na thamani sawa na ile ya mjini. Sheria imeweka utaratibu wa kupeleka maombi ya kuomba umiliki wa ardhi ya kijiji. Haki ya kumiliki ardhi kimila inaweza kutolewa kwa mtu, familia au kikundi kwa kufuata hatua zifuatazo:-

1. Mwombaji/waombaji watajaza fomu, na kuisaini. Ombi hili liambatanishwe na tamko kuhusu ardhi nyingine ambayo mwombaji anaimiliki hapa nchini.
2. Mwombaji/waombaji watoe maelezo na nyaraka zingine zitakazotakiwa na Halmashauri ya kijiji. Kama waombaji ni kikundi kinachotambulika kwa mujibu wa sheria ya kimila, fomu isainiwe na watu wasiopungua wawili wanaotambulika kama wakuu au viongozi wa kikundi hicho.
3. Malipo yaambatanishwe na fomu ya maombi na mwombaji/waombaji wapatiwe stakabadhi ya malipo.
4. Mwombaji/waombaji wasio wenyeji wa kijiji hicho waambatanishe maelezo kuhusu mipango yao ya ujenzi wa makazi ya kudumu ndani ya miezi

mitatu baada ya kupata haki ya kumiliki ardhi na kila fomu isainiwe na wanakijiji wasiopungua watano ambao hawana undugu na mwombaji.

5. Maombi yawasilishwe kwa Halmashauri ya kijiji au afisa mwenye mamlaka.
6. Maamuzi ya maombi kukubaliwa au kukataliwa yanatakiwa yatolewe ndani ya siku 90 tangu maombi yalivyopokelewa na Halmashauri ya kijiji.

**Kurejesha kugawa au kuhamisha haki ya kumiliki ardhi**

Sheria imewapa watu uhuru wa kupeleka maombi kwenye baraza la ardhi la kijiji endapo wanataka kugawa au kuhamisha haki ya kumiliki ardhi. Hata hivyo katika kufikiria maombi ya mtu binafsi ya kutaka kugawa/kutoa ardhi yake anayomiliki kihalali, Baraza la kijiji linatakiwa lihakikishe kuwa mahitaji maalum ya wanawake ya kupata ardhi yanatimizwa kwanza, ili kuhakikisha kwamba, kurejesha, kugawa au kuhamishwa kwa haki ya kumiliki ardhi hiyo hakujapangwa kwa nia ya kumdhulumu mwanamke haki yake ya kumiliki ardhi. Na pia kwamba kabla ya kutolewa maombi yoyote juu ya ardhi hiyo iliyorejeshwa, baraza linatakiwa kwanza kumuuliza mwanandoa wa mrejeshaji kama atahitaji ardhi hiyo. Endapo mrejeshaji ni mwanamume na ana mke zaidi ya mmoja basi wake zake wataulizwa kulingana na mpangilio wa nani aliyeolewa kwanza.

Vipengele vyote hivi vinampa mwanamke nafasi ya kumiliki ardhi kwa yeye kupewa hiyo ardhi kabla ardhi anayomiliki mumewe haijatolewa kwa mtu mwingine yeyote yule.

## Rehani, Upangaji na Ukodishaji

Masuala yote haya yanafuata taratibu sawa kama ilivyoelezwa hapo awali chini ya Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 kama sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002 na marekebisho ya sheria hizi ya mwaka 2004 na 2005.

## Makosa ya Jinai yaliyoainishwa katika Sheria za Ardhi 1999

Sheria zote mbili zimeeleza kuwa ni kosa la jinai kwa mtu yeyote, kutoa habari za uongo kimaandishi au kwa mdomo kuhusiana na ugawaji wa ardhi au shughuli yoyote inayohusu ardhi au jambo lolote linalohusiana na sheria hizi za ardhi. Iwapo itabainika kuwa mtu ametenda kosa lolote la aina hii, atahukumiwa kifungo kisichozidi miaka mitatu, au faini isiyozidi shilingi milioni moja au vyote viwili, faini na kifungo kwa pamoja.

## USULUHISHI NA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

Ugawaji, umilikaji wa ardhi na maamuzi yanayofanyika kuhusiana na ardhi hayakosi migogoro na migongano ya hapa na pale. Ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka na watu wote wanapata haki sawa katika kupata na kumiliki ardhi, migogoro hiyo inabidi itatuliwe kisheria. Hivyo basi Sheria hizi zote za ardhi zimeweka vyombo mbalimbali ili kushughulikia usuluhishi na utatuzi wa mingogoro hiyo. Vyombo hivi ni:-

- Baraza la Ardhi la kijiji
- Baraza la Kata
- Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya
- Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi
- Mahakama ya Rufani

**SHERIA YA MAHAKAMA ZA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI, SURA 216 (Kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002)**

Pamoja na Sheria mbili za Ardhi kutungwa na Bunge letu, pia imetungwa na kupitishwa Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, namba 2 ya mwaka 2002 Sura ya 216 iliyoanza kutumika hapa nchini toka tarehe 1 Oktoba, 2003. Sheria inaainisha vyombo mbalimbali vinavyoshughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi.

**Vyombo hivi ni:-**

**1. Baraza la Ardhi la kijiji**

- Litaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 na litakuwa na wajumbe saba. Watatu kati yao lazima wawe wanawake.
- Koramu ya mkutano wa Baraza hili ni wajumbe wanne ambao kati yao wawili ni lazima wawe wanawake.
- Litaendesha mikutano yake kwa njia ya upatanishi.
- Litapokea mashauri yote yanayohusu ardhi ya kijiji.
- Mawakili hawaruhusiwi kuwakilisha wateja wao katika baraza hili.

**2. Baraza la Kata**

- Litaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabaraza ya Kata ya mwaka 1985 Sura ya 206 kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002 na litakuwa na wajumbe wasiopungua wanne na wasiozidi wanane.
- Litaendesha mikutano yake kwa njia ya upatanishi.
- Litapokea mashauri ambayo thamani yake haizidi shilingi milioni 3 yanayohusu ardhi ndani ya mipaka ya kata hiyo.
- Litapokea rufani kutoka Baraza la Ardhi la kijiji kilichopo katika kata hiyo.
- Kikao halali cha Baraza kinachoweza kutoa maamuzi ya suala la ardhi ni wajumbe watatu na kati

yao angalau mmoja lazima awe mwanamke.

- Mawakili hawaruhusiwi kuwakilisha wateja wao katika Baraza hili.

**3. Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya**

- Hupokea mashauri ambayo thamani yake haizidi shilingi milioni 50 kwa mali isiyohamishika na isiyozidi shilingi miloni 40 kwa mali inayohamishika.
- Hupokea rufani kutoka Baraza la Kata.
- Rufani ziwasilishwe katika Baraza hili ndani ya siku 45 toka maamuzi ya Baraza la Kata.
- Mwenyekiti ataendesha mashauri akiwa na Wazee wawili wa Baraza.
- Mwenyekiti lazima awe mwanasheria.
- Mawakili wanaruhusiwa kuwakilisha wateja wao katika Baraza hili.
- Litasaidia utekelezaji wa maamuzi ya Baraza la Kata yatakayohusu masuala ya ardhi.

**4. Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi**

- Hupokea mashauri ambayo thamani yake ni zaidi ya shilingi milioni 50 kwa mali isiyohamishika na inayozidi shilingi milioni 40 kwa mali inayohamishika.
- Hupokea na kusikiliza rufani ya mashauri kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya.
- Rufani zipelekwe katika mahakama hii ndani ya siku 60 tangu shauri lilipomalizika.
- Mawakili wanaruhusiwa kusimamia wateja wao katika mahakama hii.

**5. Mahakama ya Rufani**

Itapokea rufani kutoka Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Sheria ya Mahakama ya Rufani ya mwaka 1979 sura ya 414 kama, sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002 ambayo inalazimisha:-

4. Kutoa taarifa kwa Msajili wa Mahakama Kuu kuwa kuna nia ya kukata rufani ndani ya siku 14 toka siku ya hukumu ya Mahakama Kuu. Taarifa hii hupelekwa kwa upande mwingine ndani ya siku 7 toka tarehe taarifa hiyo iliposainiwa na Msajili wa Mahakama Kuu.
5. Kuomba ruhusa ya kukata rufani ukionesha hoja ya kisheria unayotaka Mahakama ya Rufani ikatolee maamuzi. Ruhusa hii huombwa Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi.

## Changamoto

Wanawake wajitokeze kwa wingi kupata nafasi hizi ili kuhakikisha kuwa maslahi yao katika ardhi yanaangaliwa ipasavyo. Hatuna budi kuelewa kwamba hakuna mtu mwingine atakayetetea maslahi ya wanawake katika kumiliki ardhi isipokuwa wanawake mwenyewe. Ni matumaini yetu kuwa iwapo jamii itaelimika juu ya masuala ya ardhi basi tunaweza kutoa/kuheshimu nafasi ya mwanawake kumiliki ardhi. Ni jukumu la kila mwananchi na serikali kwa ujumla wakiwemo maafisa wa ardhi na kamati mbalimbali za kushughulikia masuala ya ardhi, kuhakikisha kwamba haki ya mwanamke katika kumiliki ardhi inazingatiwa ili tuweze kusukuma gurudumu la maendeleo kwa pamoja.

## Hitimisho

Ni ukweli usiopingika kuwa wanawake hawapewi haki sawa na wanaume katika kumiliki ardhi. Pia juhudi zozote zinazofanywa kisheria kwa lengo la kuondoa ubaguzi wa kijinsia, hasa ambapo suala lenyewe linagusa mila na desturi ambazo zimekuwepo toka enzi na enzi, zinachukua muda mrefu kubadilika kiasi cha kukatisha tamaa. Hata hivyo hii isituvunje moyo kwani siku moja jamii itaelewa umuhimu wa kuachana na mila na desturi zinazowabagua wanawake. Tunaamini kabisa kuwa juhudi tutakazozielekeza katika kuelimisha jamii nzima kuhusu sheria hizi mpya zitazaa

matunda mazuri. Hivyo basi, ni jukumu la kila mtu kuielimisha jamii juu ya sheria za ardhi.

Kuwepo kwa Sheria hizi mpya za Ardhi kumetoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika kuomba, kutumia na kumiliki ardhi, haki ambayo kila mmoja anatakiwa kuilinda. Kwa kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika kutumia ardhi kwenye masuala na juhudi za uzalishaji mali na kwa kuwa pia nafasi ya umiliki ardhi itachochea nguvu ya uzalishaji mali, pato la taifa litaongezeka na hivyo kupunguza umaskini katika nchi yetu.

**Maswali kwa wasomaji**

1. Eleza nafasi ya mwanamke katika kumiliki ardhi.

2. Eleza upungufu unaojitokeza katika utekelezaji wa Sheria za Ardhi.

3. Njia zipi zitumike ili Sheria za Ardhi zijulikane kwa jamii?

# SURA YA PILI

# SHERIA YA NDOA

## UTANGULIZI

Ndoa ni taasisi ya zamani sana katika jamii. Ni kitu kilichoanza tangu mwanadamu alipoanza kuishi. Kwa kuwa ndoa ndio chimbuko la jamii yoyote ile, kila jamii ina utaratibu wa kufuata ili ndoa iwepo na jinsi ya kudumisha mahusiano yanayotokana na ndoa hiyo. Kabla ya ujio wa wageni, Watanganyika walikuwa wakiongozwa na taratibu za kimila katika masuala ya ndoa. Kila kabila au jamii walikuwa na utaratibu wao. Kuja kwa wageni hapa Tanzania kuliandamana na taratibu ngeni kuhusu mambo yanayohusu ndoa. Waarabu walipokuja walikuja na sheria na taratibu zao ambazo zilienda pamoja na imani ya dini ya Kiislam. Lakini kwa upande wa ndoa sheria zao hazijaingilia sana taratibu za kimila kuhusu ndoa. Wajerumani na hata Waingereza walikuja na mfumo wao. Mfumo huu ulienda pamoja na imani ya dini ya Ukristo waliyoileta iliyomtaka mwanaume awe na mke mmoja tu. Hii ilikuwa ni kinyume na utaratibu au mfumo wa kimila ambapo mtu aliweza kuoa wake wengi kadiri ya uwezo wake. Pia katika imani ya Kiislamu waumini wake waliagizwa kuoa wake si zaidi ya wanne kwa wakati mmoja. Kadhalika imani hizi za Ukristo na Uislamu zilikataza mtu kuoa au kuolewa na mtu wa dini tofauti.

Ilipofika mwaka 1921 serikali ya kikoloni ilitunga sheria iliyozipa mahakama walizozianzisha mamlaka ya kushughulikia masuala ya ndoa. Mahakama zilizoanzishwa zilikuwa za aina mbili, yaani mahakama za kimila na mahakama za serikali kuu ya kikoloni. Mashauri yaliyohusu ndoa zilizofungwa kimila yalipelekwa katika mahakama za Kimila. Mahakama hizi zilikuwa zinawahudumia wale wenye asili ya Kiafrika tu. Kama ndoa ilikuwa imefungwa

kikristo mahakama za kienyeji hazikuwa na mamlaka ya kusikiliza ndoa hiyo. Shauri kama hilo lilikuwa linapelekwa katika mahakama za serikali.

Mahakama za serikali pia zilikuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri lolote toka kwa mtu yeyote. Zilipewa uwezo wa kutafsiri na kutumia sheria za mila ikiwa waliona sheria za mila hazipingani na utamaduni na sheria zao.

Mwaka 1963 serikali iliondoa mfumo wa mahakama za kikoloni na kuleta muundo mpya. Pamoja na mabadiliko hayo sheria za mila kuhusu ndoa ziliendelea kutumika pamoja na mafundisho ya dini kuhusu ndoa. Mwaka huo huo wa 1963 serikali ilitangaza Sheria ya Hali za Watu. Sheria hii ilijaribu kukusanya taratibu mbali mbali za mila toka karibu makabila yote ya Tanganyika na kuziweka katika Tangazo la Serikali na. 279 la mwaka 1963.

Pamoja na mkusanyo huu wa sheria za mila, mfumo mpya wa mahakama uliendelea kutumia taratibu karibu zile zile za Kiingereza (kikoloni). Kwa mfano, pale ambapo sheria fulani ya mila ilionekana kwenda kinyume au inapingana na mwelekeo wa serikali, sheria hiyo ilibatilishwa. Pamoja na msimamo huu wa serikali wa kupitisha mfumo mpya wa mahakama, dini zote ziliendelea kuhimiza waumini wao kufuata dini zao zinavyosema kuhusu ndoa. Tofauti na utatanishi ulijitokeza miongoni mwa waumini wa dini hizo ambao ulisababisha serikali kutunga Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Sheria hii ndiyo itakayojadiliwa kwa undani katika Sura hii.

## SEHEMU YA KWANZA

### Maana ya Ndoa

Ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao.

**Vigezo vya kuzingatia ili wanaotaka kufunga ndoa wakubaliwe kisheria kufunga ndoa.**

**Sheria inatamka vigezo vifuatavyo:-**

**(a) Muungano lazima uwe wa hiari**

Mwanaume na Mwanamke wawe wameamua kuishi pamoja kwa ridhaa yao wenyewe. Hii inamaanisha kusiwe na kulazimishwa au kuhadaiwa kwa aina yoyote kwani muungano kama huo utakuwa batili kisheria. Ni kosa la jinai kushiriki katika shughuli ya ndoa ambayo mmoja wapo au wote wanalazimishwa kufunga ndoa.

**(b) Muungano uwe ni kati ya mwanamke na mwanaume.**

Wanaotaka kuoana ni sharti wawe mwanaume na mwanamke.

Muungano wa watu wa jinsi moja hata kama ni wa hiari muungano huo hautambuliki kisheria. Pia mtu huhesabika mwanamke au mwanaume kutokana na sehemu za siri alizozaliwa nazo na siyo alizozipata baadaye. Jamii inachukuliwa kuwa ndoa ni njia pekee ya kujiongeza na kujipanua. Kuongezeka huku ni kwa kuzaa watoto. Kwa hali hiyo ili kupata watoto ni lazima ndoa iwe kati ya mwanaume na mwanamke.

**(c) Muungano huo uwe unakusudiwa kuwa wa kudumu**

Pamoja na kuwa mwanamke na mwanaume wameamua kuishi pamoja kwa hiari yao lakini kama muungano huo siyo wa kudumu basi hautambuliki kisheria kama ndoa. Muungano ni lazima uwe wa kudumu maisha yote au kama mmoja wao atafariki au kama ndoa itakumbwa na matatizo na mahakama ikaona ni bora kuivunja ndoa hiyo kisheria.

### (d) Wafunga ndoa wasiwe maharimu

Maharimu ni watu walio na mahusiano ya karibu ya damu au kindugu.

Wale wanaoamua kufunga ndoa wasiwe na uhusiano wa karibu kindugu. Inakatazwa mtu kuoa au kuolewa na mzazi wake, mtoto au mjukuu wake, kama ni dada yake, mama au shangazi au baba wa mjomba wake, baba au mama wa kambo na mwanaye aliyemuasili kuwa mtoto wake.

### (e) Wafunga ndoa wawe wametimiza umri unaokubalika kisheria

Mwanamke na mwanaume wanatakiwa wawe wametimiza miaka 18 ili kufunga ndoa. Hata hivyo mwanamke anaweza kuolewa akiwa na umri wa chini ya miaka 18 lakini sio chini ya miaka 15 kama atapata idhini ambayo hutolewa na baba na kama hayupo ni mama au kama wote wamefariki idhini itatolewa na mlezi wa binti huyo. Kama wote hawa wamefariki basi hatahitaji idhini.

**Hoja**

Sheria ya Makosa ya kujamiiana inatamka wazi kuwa mwanamume yeyote anayefanya mapenzi na binti mwenye umri chini ya miaka 18 ambaye siyo mkewe atakuwa amebaka. Je mahakama chini ya kifungu cha hapo juu itakuwa inakubali kubaka??

Kuna mazingira fulani mahakama inaweza kutoa idhini kwa binti kuolewa akiwa na miaka 14 lakini si chini ya hapa ikiwa ataonekana kwa mfano ana mimba. Pia mwanaume anaweza kuruhusiwa na mahakama kuoa akiwa chini ya miaka 18 lakini si chini ya miaka 16 kama ataonesha kuelewa jukumu lake kama mtu mzima. Lakini hii ni pale ambapo kuna tatizo kama la kumpa msichana mimba ndipo mahakama inaweza ikatoa idhini. Katika

ombi la kuoa la SHABIRI A.M VIRJI (1971) HCD No. 407 la Mahakama Kuu ya Tanzania, mwombaji alikuwa na miaka 16 lakini alimpa mimba binti wa miaka 18. Mahakama katika kuchunguza ombi la mvulana la kuoa ilitoa kibali kwa sababu wote wawili walipendana na wazazi wao hawakuwa na kipingamizi cha wao kuoana.

**(f) Kusiwe na ndoa inayoendelea**

Kama mwanamke ana ndoa inayoendelea na inatambulika kisheria haruhusiwi kufunga ndoa nyingine (Polyandry). Kadhalika kama mwanamume ana ndoa ya mke mmoja au kama ni Mwislamu ana wake wanne hataruhusiwa kufunga tena ndoa.

**(g) Kusiwe na kipingamizi**

Pasiwe na kipangamizi chochote kilichowekwa kwa mfungishaji ndoa ndani ya siku 21 baada ya ndoa kutangazwa na kabla siku y a kufunga ndoa. Mfungishaji anapopokea pingamizi anapaswa asitishe ufungishaji ndoa hadi pale pingamizi litakapoondolewa.

**(h) Mfungishaji ndoa kutokuwa na mamlaka**

Ndoa ni lazima ifungishwe na mfungishaji mwenye uwezo kisheria kufanya hivyo. Ili mfungishaji ndoa awe na uwezo kisheria inabidi awe amesajiliwa na Msajili wa ndoa na kupewa leseni inayomruhusu kufungisha ndoa.

**(i) Kutokuwepo kwa wafunga ndoa**

Kama ndoa imefungwa bila ya wafunga ndoa wote kuwepo basi ndoa hiyo haitambuliki kisheria. Hata hivyo sheria inaruhusu ndoa kufungwa ikiwa mmoja wa wafunga ndoa hayupo lakini amewakilishwa na mtu ambaye alikuwepo wakati mfunga ndoa ambaye hayupo, alipotoa ridhaa yake ya kuoa au kuolewa.

**(j) Mashahidi wa ndoa**

Ili ndoa itambulike kisheria ni lazima ishuhudiwe na mashahidi wasiopungua wawili ambao wanaruhusiwa kisheria yaani umri wao usipungue miaka 18 na wafahamu kinachosemwa na kutendeka wakati wa kufunga ndoa.

**(k) Kuwa katika Eda**

Eda ni kipindi cha kukaa ndani kinachotolewa kwa mwanamke wa Kiislamu aliyeachika katika ndoa au aliyefiwa na mumewe, ili taratibu fulani za kidini zifanyike.

Kama mwanamke ambaye ndoa ilifungwa Kiislamu anaolewa kipindi cha Eda hakijaisha basi ndoa hiyo ni batili. Kama atabadili dini baada ya kufiwa au kupewa talaka masharti ya Eda hayatambana.

## SEHEMU YA PILI

### Aina za ufungaji wa Ndoa na Taratibu za Kufuata

Kabla ya kufunga ndoa utaratibu ufuatao lazima uzingatiwe:

**(a) Kutoa Taarifa ya nia ya kuoana**

Kwanza kama mwanamke na mwanamume wanataka kufunga ndoa ni wajibu taarifa ya nia ya kufunga ndoa itolewe kwa mfungishaji ndoa siku 21 kabla ya siku ya kufunga ndoa. Taarifa hiyo ioneshe mambo yafuatayo:-

(i) Majina kamili na umri wa hao wanaotaka kuoana.

(ii) Uthibitisho kwamba hakuna kipingamizi dhidi ya hiyo ndoa wanayotarajia kufunga.

(iii) Majina kamili ya wazazi wao na sehemu wanakoishi.

(iv) Hadhi ya wafunga ndoa. Yaani kama ni mwanamke ifahamike kama hajaolewa, ametalikiwa au ni mjane na mwanamume pia anapaswa kuwa hajaoa, au ana mke/wake wengine (hii ni kwa ndoa za kiserikali na Kiislamu) au kama ametaliki.

(v) Kama muolewaji ana umri chini ya miaka 18, jina la mtu aliyetoa idhini ya yeye kuolewa kama yupo lionyeshwe.

(vi) Kama ni ndoa ya Kiserikali au Kiislamu hapana budi kueleza kama ndoa ni ya wake wengi au inatazamiwa kuwa ya wake wengi na majina ya wake waliopo yatajwe. Pia katika fungu hili kama mtu anataka ndoa iwe ya mke mmoja anapaswa kueleza.

### (b) Kutangaza nia ya kufunga Ndoa

Baada ya taarifa yenye maelezo haya kufikishwa kwa mfungishaji ndoa, yeye atawajibika kuitangaza nia hii ya kufunga ndoa. Sababu ya kufanya hivyo ni ili kama kuna mwenye kipingamizi na ndoa hiyo atoe taarifa. Matangazo haya hutolewa kulingana na aina ya ufungishaji wa ndoa. Kama ndoa inatarajiwa kufungwa kidini, matangazo hutolewa sehemu za ibada. Kama ni ndoa ya Kiserikali tangazo litabandikwa nje ya ofisi ya Msajili wa Ndoa ambaye ni Mkuu wa Wilaya. Vipingamizi vya ndoa viko vya aina mbili, cha kwanza ni kile cha kisheria yaani kama ndoa itakayofungwa itakuwa batili. Kipingamizi cha pili ni kama muoaji ana mke au wake wengine tayari, hivyo mke au wake wanaweza kutoa kipingamizi kama uwezo wa muoaji kifedha ni mdogo kiasi

kwamba kuongeza mke mwingine kutazidisha taabu.

**Nini hufanyika pindi kukiwa na kipingamizi**

Mfungishaji ndoa anapopokea taarifa ya kupinga ndoa isifungwe, atapeleka taarifa hiyo kwenye Baraza la Usuluhishi la Ndoa. Huko aliyeweka pingamizi pamoja na yule anayetaka kuoa au kuolewa wataitwa na kila mmoja atajieleza. Baada ya kusikiliza pande zote Baraza lina uwezo wa kuamua ndoa hiyo ifungwe au isifungwe na mfungishaji ndoa atafuata uamuzi wa Baraza. Kama mtu atatoa kipingamizi cha uongo na ikithibitika hivyo anaweza kushitakiwa na akitiwa hatiani adhabu yake anaweza kufungwa kifungo kisichozidi miaka mitatu. Baada ya kipengele hiki kutimizwa ndoa inaweza kufungwa.

**Aina za ndoa**

Kuna aina mbili za ndoa;

**(a) Ndoa ya mke mmoja**

Huu ni muungano unaoruhusu mwanaume kuoa si zaidi ya mke mmoja. Mfano, ndoa ya kikristo.

**(b) Ndoa ya zaidi ya mke mmoja**

Huu ni muungano unaoruhusu mwanaume kuoa mke zaidi ya mmoja. Mfano, ndoa za Kiislamu na ndoa za kimila

Sheria ya Ndoa inatambua aina 3 za ufungaji wa ndoa yaani kiserikali, kidini na kimila.

**(a) Ndoa ya Kidini**

Ndoa hii hufungwa kwa mujibu wa taratibu ya dini inayohusika. Ni lazima masharti yote yatimizwe kisheria, taarifa ya nia ya kufunga ndoa itolewe, ndoa ifungwe mahali pa wazi panapokubalika kisheria na mfungishaji awe na mamlaka hayo kisheria.

**(b) Ndoa ya Kiserikali**

Ndoa hii hufungwa mbele ya Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye

Msajili wa Ndoa. Ndoa itafungwa katika Ofisi ya Msajili au mahali pengine popote palipotajwa katika leseni yake ya kufungisha ndoa.

### (c) Ndoa ya Kimila

Ndoa inaweza kufungwa kimila iwapo mmoja wa wafunga ndoa au wote wawili wanafuata sheria za mila za kabila fulani. Mdhamini wa ndoa za kimila ni Katibu Tarafa. Ndoa ya kimila hufungishwa na mtu anayetambulika kimila kuwa ana uwezo huo. Ni muhimu sana Katibu Tarafa kuhudhuria kwenye ufungishaji huo wa ndoa kwani ndiye atakayehusika na kuleta vyeti vya ndoa kutoka kwa Msajili.

### Ufungaji Ndoa nje ya Nchi

Waziri wa Sheria ana mamlaka ya kuteua baadhi ya maofisa ubalozi kuwa wasajili wa ndoa. Ni lazima msajili aridhike kuwa masharti yote yametimizwa ndipo afungishe ndoa. Kuna masharti ya nyongeza kama angalau mmoja wa wafunga ndoa hawa ni Mtanzania. Pia kama mmoja wa wafunga ndoa si Mtanzania ni lazima Msajili aridhike kuwa ndoa inayokusudiwa kufungwa itatambulika kisheria katika nchi ambayo huyo mmoja wa wafunga ndoa ni mkazi. Utaratibu unaotumika kufungisha ndoa hizi ni sawa na ule unaotumika katika kufungisha ndoa za Kiserikali.

### Dhana ya Kuchukulia Ndoa

Kuna dhana inayokanushika kuwa mwanamume na mwanamke wakiishi pamoja huweza kuchukuliwa kuwa ni mke na mume mbele ya sheria japokuwa hawakuwahi kufunga ndoa. Ili dhana hii iwepo ni lazima yafuatayo yathibitishwe.

(1) Lazima ithibitike kwamba mwanamke na mwanamume wameishi pamoja kwa muda wa miaka 2 au zaidi kwa mfululizo.

(2) Lazima ithibitike kuwa umma unaowazunguka unawachukulia na kuwapa heshima kama mke na mume.

(3) Lazima ithibitishwe kuwa watu hao walikuwa na uwezo wa kuwa mke na mume wakati walipoanza kuishi pamoja na kama walikuwa na umri uliokubalika kisheria.

(4) Ni lazima pia ithibitishwe kuwa kati ya hao wawili au wote hakuna aliye na ndoa inayoendelea.

## SEHEMU YA TATU

### Ndoa Batilifu na Sababu zinazoweza kuifanya Ndoa kuwa Batilifu

Ndoa batilifu ni ndoa ambayo itachukuliwa kisheria kuwa ni ndoa halali hadi hapo amri ya kuivunja itakapotolewa. Ndoa batilifu ni halali kama ndoa nyingine isipokuwa ina kasoro fulani. Wanandoa katika ndoa hii wana haki na wajibu sawa kama ilivyo katika ndoa nyingine zisizo na kasoro. Kadhalika watoto waliozaliwa katika ndoa ya namna hii ni halali na wana haki zote kisheria.

### Ni vitu gani vinafanya Ndoa kuwa Batilifu?

Sababu zinazoweza kufanya ndoa kuwa batilifu ni:

**1. Maradhi ya zinaa**

Kama wakati wa kufunga ndoa mmoja wa wafunga ndoa alikuwa na maradhi ya zinaa na yule asiye na ugonjwa kama wakati wa kufunga ndoa alikuwa hajui lolote kuhusu maradhi hayo anaweza kulalamika mahakamani na ndoa ikavunjwa.

**2. Kukataa kwa makusudi kuitimiliza ndoa**

Kama baada ya kufunga ndoa mmoja wa wana ndoa atakataa kutimiliza ndoa kwa makusudi anayekataliwa ana haki ya

kuomba mahakama kuvunja ndoa hiyo. Maingiliano ya kimwili yanayotambulika kisheria ni yale yanayofanyika siku ya ndoa na kuendelea na siyo kabla ya ndoa. Kukataa kutimiliza ndoa kunakuwa sababu ya kubatilisha ndoa ikiwa mwenye kukataa hana sababu yoyote ya msingi na mwenye kukataliwa ametumia kila mbinu kumshawishi aliyekataa lakini ikashindikana.

### 3. Mimba ya mwanaume mwingine

Kama wakati wa kufunga ndoa mke atathibitika kuwa ana mimba aliyopata kwa mwanaume mwingine, mume anaweza kuiomba mahakama ivunje ndoa hiyo. Kama itathibitika kuwa mume alijua hiyo hali wakati wa kufunga ndoa, lalamiko lake halitasikilizwa.

### 4. Wazimu au kifafa cha vipindi

Mmoja wa wafunga ndoa kama ana wazimu au kifafa cha kurudia rudia na mwenzake alikuwa hajui hiyo hali wakati wa kufunga ndoa, atakuwa na haki ya kuiomba mahakama kuivunja ndoa hiyo. Ieleweke kuwa ugonjwa ni lazima uwe unarudia rudia na siyo mtu awe aliugua na akapona.

### 5. Kushindwa kutimiliza ndoa

Kama mmoja wa wana ndoa atashindwa kuitimiliza ndoa basi ndoa hiyo inaweza kubatilishwa. Kwa mwanaume kama anashindwa kuitimiliza ndoa basi ndoa hiyo inaweza kubatilishwa. Kama anashindwa kuitimiliza ndoa kwa sababu ya kukosa nguvu za kiume basi mke ana haki ya kuomba mahakama kuibatilisha ndoa. Ili kukosa nguvu za kiume kuwe sababu ya kubatilisha ndoa ni lazima ithibitike kuwa hali hiyo ilitokea kabla au wakati wa kufunga ndoa na siyo baada ya kufunga ndoa. Ili ndoa iweze kubatilika ni lazima kukosa nguvu huko kuthibitishwe na daktari kuwa hakuponi au

kunapona lakini mwanamume hataki matibabu. Pia mwanamke anaweza kuwa na maumbile ambayo yanaweza kufanya ndoa ishindwe kutimilizika. Ikithibitika hali hii inatibika lakini mwanamke hataki tiba mwanamume anaweza kuomba ndoa kubatilishwa.

**Muda wa kupeleka mahakani maombi ya kubatilisha ndoa.**

Ili mahakama iweze kusikiliza shauri la kuomba kubatilisha ndoa ni lazima shauri hilo lipelekwe mahakamani haraka. Kama shauri litakwenda mahakamani baada ya mwaka mmoja tangu tarehe ya ndoa, mahakama haitalipokea. Pia ni lazima ithibitike kuwa mlalamikaji alikuwa hajui kasoro hiyo wakati wa kufunga ndoa na baada ya kuigundua kasoro hiyo hajawahi kuingiliana na mwenzie.

Ndoa batilifu huvunjwa na mahakama pekee baada ya kupokea malalamiko toka kwa mmoja wa wanandoa. Kama hakutakuwa na malalamiko yatakayopelekwa mahakamani na anayeathirika na kasoro hizo, ndoa hiyo itadumu ama labda mpaka mmoja afariki au mpaka talaka itolewe na mahakama kama kuna maombi ya kuvunja ndoa hiyo.

**Ndoa batili na sababu za kuzifanya kuwa batili.**

Ndoa batili ni ile ambayo kisheria si halali na inahesabiwa kuwa hakuna ndoa kutokana na ubatili wa shughuli yote.

Sababu zinazofanya ndoa kuwa batili.

- Iwapo mwanamke ana umri chini ya miaka 15 na hakuna kibali cha mahakama.
- Iwapo wanandoa ni maharimu.

- Kama kuna mmojawapo ana ndoa inayoendelea ambapo anazuiwa kuingia katika ndoa nyingine mfano mwenye ndoa ya kikristu, muislamu ambaye tayari ana wake wanne au mwenye ndoa ya kiserikali/kiislamu ambaye wakati wa kufunga ndoa alisema ni ndoa ya mke mmoja.
- Iwapo mahakama au baraza la usuluhishi umekataza ndoa isifungwe lakini ndoa ikafungwa.
- Kama wote au mmoja wao hakuingia kwenye ndoa bila hiari.
- Kama wanandoa wote hawakuwapo kwenye tukio la kufunga harusi.
- Kama wanandoa kwa kufahamu kuwa mfungishaji hana mamlaka lakini wakamwacha afungishe ndoa.
- Iwapo ufungishaji ndoa haukushuhudiwa na mashahidi.
- Kama ndoa inalenga kuwa ya muda.
- Iwapo mwanamke yuko katika eda.

**Kugeuza Ndoa**

Watu waliooana wana uhuru wa kugeuza ndoa yao pale wanapofuata taratibu zilizowekwa kisheria. Kabla ya kufanya uamuzi wa kugeuza ndoa ni budi wanandoa wakubaliane kuhusu uamuzi huo. Kitendo cha kugeuza ndoa hufanywa mbele ya Hakimu wa Wilaya au Jaji ambapo wanandoa watatoa tamko la maandishi lenye saini zao na Hakimu au Jaji aliyeshuhudia naye huweka saini yake.

Katika kugeuza ndoa, ndoa ya kiserikali, ya kimila au ya Kiislamu inaweza kugeuzwa kuwa ya mke mmoja kama kabla ya kugeuza ilikuwa ni ndoa ya wake wengi.

Ikumbukwe kuwa kubadilisha dini pekee hakubadilishi hadhi ya ndoa. Vile vile ndoa ya kikristo haiwezi kugeuzwa kuwa

ya wake wengi wala ndoa ya wake wengi ambayo ina wake zaidi ya mmoja kuwa ya mke mmoja

## SEHEMU YA NNE

### Haki na Wajibu katika Ndoa

Baada ya taratibu zote za ndoa kufuatwa na kwamba ndoa haina kasoro yoyote, mke ana haki mbalimbali anazostahili kuzipata kisheria. Haki hizo ni kama ifuatavyo:-

### Matunzo

Mke au wake wana haki ya kutunzwa na mumewe/mume wao kwa kuwapatia mahitaji muhimu kama chakula, malazi, mavazi, matibabu n.k kulingana na uwezo wa kumtunza mke/wake.

Kama ni kijijini mume anapaswa kumpa mke jembe, kumwonyesha mahali pa kulima na kumsaidia kukata miti na visiki. Iwapo mume ana mke zaidi ya mmoja ana wajibu wa kuwatunza wote bila ya upendeleo. Pia mume ana wajibu wa kuwatunza watoto wote waliozaliwa ndani ya ndoa.

### Kumiliki Mali

Mke ana haki ya kumiliki mali aliyoipata kabla ya ndoa na hata wakati wa ndoa kama ameipata kwa fedha zake mwenyewe au kupewa zawadi. Mke pia ana haki ya kuingia mikataba, kufungua madai dhidi ya wadeni wake au kudaiwa, kununua mali au kuiuza. Kwa kuwa mume nae ana haki hizo hizo, hii inamaanisha kuwa ndoa peke yake haibadilishi haki ya kumiliki mali kati ya mke na mume. Pamoja na hali hii mke na mume wanaweza kukubaliana kuwa mali ambazo kila mmoja alikuwa nazo kabla ya ndoa au wakati wa ndoa ziwe zao kwa pamoja.

### Mke kukopa kwa dhamana ya mumewe

Kwa kuwa katika hali ya kawaida mume ana wajibu wa

kumtunza mke na watoto kuna wakati inawezekana mume akasafiri kwa muda mrefu na hakuacha fedha au alizoacha zimekwisha, au mume amemtoroka mke na kumwachia watoto. Mke ana haki ya kukopa fedha kwa jina la mumewe au kuweka rehani mali ya mumewe. Mke ana uwezo wa kutumia mali ya mumewe ambayo inahamishika au kutumia fedha za mumewe zilizoko mikononi mwake kwa ajili ya kununulia mahitaji ya muhimu kwa ajili yake na watoto wake ni halali kisheria.

Haki hizi zinakuwepo kama mke na mume wanaishi pamoja au kama wametengana kwa mapatano kuwa mume atatoa matunzo na mume amepuuzia mapatano hayo. Jambo la kuzingatia kwa makini hapa ni kuwa ili haki ya kutumia mali ya mume iweze kuwapo ni lazima mahitaji yanayonunuliwa yawe ni yale ambayo kama mume mwenyewe angekuwepo, angekuwa na uwezo wa kuyanunua kulingana na pato lake.

**Haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa**

Nyumba ya ndoa ni nyumba ambayo mume na mke wanaishi wakati wa ndoa. Hata kama wana nyumba nyingi ni nyumba moja tu ndiyo inayochukuliwa kama nyumba ya ndoa. Pamoja na kuwa nyumba ya ndoa inaweza kuwa mali binafsi ya mke au mume, nyumba hiyo haiwezi kuuzwa, kuwekwa rehani au kuchukuliwa na mtu mwingine kama zawadi bila ya makubaliano ya wote wawili. Ikiwa mume atafanya chochote kwenye nyumba hii bila ya makubaliano na mke, mke atakuwa na haki ya kuishi katika nyumba hiyo hadi hapo Mahakama itakapotoa maamuzi ya kuvunja ndoa hiyo, kutengana au amri ya matunzo. Kadhalika mume naye anayo haki hiyo hiyo iwapo mke ndiye mwenye

nyumba na anataka kumfukuza mumewe. Ikumbukwe kuwa nyumba ya ndoa siyo lazima iwe nyumba ambayo mmoja wao amenunua ama amejenga. Hata kama nyumba ni ya kupanga bado itatambulika kisheria kama nyumba ya ndoa.

**Mali iliyopatikana wakati wa ndoa**

Mali ya mke au mume iliyopatikana kutokana na jasho lao wote wawili ni mali yao kwa pamoja hata kama juhudi zao au jasho lao katika kupata mali hizi si sawasawa. Lakini pamoja na hayo kuna dhana inayokanushika kuwa kama mali hii imeandikishwa kwa jina la mmoja wao basi ni mali yake. Ni wajibu wa yule anayedai kuthibitisha kuwa ni mali ya pamoja na kwamba mali imeandikishwa kwa jina la mwenzake. Kuhusu mali iliyopatikana kwa pamoja katika kesi ya **ABDALLA SHAMTE V AUSA Na. 9 1972 HCD** mke na mume walikubaliana kujenga nyumba za kupangisha kutokana na kipato cha mishahara yao. Baada ya muda waliweza kujenga nyumba tatu. Walipoachana kwa talaka mume alikataa kumpa mkewe mojawapo ya nyumba hizo tatu. Mke alifungua kesi ya madai ya kudai Shs. 33,000/- na alipatiwa kama alivyoomba.

Wakati wa kugawa mali ni lazima Mahakama iwe imeridhika na mambo yafuatayo.

(i) Kuwa mali inayogawanywa iwe imepatikana kutokana na juhudi za pamoja kati ya mke na mume.
(ii) Kuwa mali inayogawanywa inatokana na kuwepo kwa ndoa.
(iii) Kwamba mali inayogawanywa imepatikana wakati wa ndoa.

Kipengele cha kwanza kiliwahi kuleta matatizo katika kutafsiri ni nini maana ya “juhudi za pamoja”. Kazi za ndani za mke

hazikuhesabiwa kama juhudi za pamoja.

Tafsiri iliyong'ang'aniwa kwa muda mrefu ni ile ya kuwa mali iliyopatikana kutokana na juhudi za pamoja ni ile ambayo kila mmoja wao amechangia katika kuipata.

Mwaka 1983 Mahakama ya Rufani ya Tanzania iliamua kuwa juhudi za pamoja inamaanisha pia kazi za ndani anazozifanya mke wakati ndoa inaendelea. Uamuzi huo ulitolewa katika kesi ya **Bi. HAWA MOHAMED dhidi ya ALI SEFU,** ambapo mume alikuwa anadai kuwa kwa vile mke alikuwa mama wa ndani basi hakuchangia chochote katika mali iliyochumwa wakati wa ndoa.

**Mjane kuwa na uhuru wa kuishi anapotaka pindi afiwapo**

Pale mke anapofiwa na mumewe ana uhuru wa kuendelea kuishi au kutoishi katika nyumba waliyokuwa wakiishi na mumewe. Pia ana uhuru wa kuolewa tena au kutokuolewa. Katika makabila yako yaliyo na desturi za kurithi wake, mwenye kurithi mke anapaswa afuate taratibu za kisheria za kufunga ndoa na cheti kitatolewa.

**Kipigo kwa mwanandoa**

Bila kujali dini, kabila au jinsi hakuna mwanandoa mwenye haki ya kumpiga mwenzake. Yaani mke haruhusiwi kumpiga mume na mume hali kadhalika haruhusiwi kumpiga mke. Hili ni kosa la jinai kama ambavyo umempiga mtu yeyote yule.

**Maswali**

1. Ndoa ni nini?

2. Ni mambo gani mtu anapaswa kutilia maanani ili aweze kuruhusiwa kufunga ndoa.

3. Ni mambo yapi yanaweza kufanya ndoa kuwa batilifu?

4. Bwana Joseph Anthony

yuko Nigeria na anataka kufunga ndoa mjini Lagos na Bi Nancy Ntehene wa Tanzania. Je afanyeje?

5. Bwana Sikujua baada ya kuishi na Sikudhani kwa miaka 10 ameamua kumfukuza kwa madai kuwa hajafunga naye ndoa. Je! Sikudhani ana haki gani kisheria. Na kama zipo ni kwa nini?

# SURA YA TATU

# TALAKA

## UTANGULIZI

## SEHEMU YA KWANZA

### Maana ya Talaka

Sheria inayosimamia masuala ya talaka ni sheria ya Ndoa ya 1971. Na kwa mujibu wa sheria hiyo, Talaka ni ruhusa ya kisheria ambayo mume au mke hupewa wakati anapomwacha mwenzie.

### Chombo chenye mamlaka ya kutoa talaka

Chombo pekee chenye uwezo wa kuvunja ndoa ni mahakama. Kwa kawaida mahakama hutoa talaka kwa ndoa ambayo imedumu kwa kipindi cha miaka miwili au zaidi. Lakini mahakama inaweza kutoa talaka hata kama ndoa haijadumu kwa kipindi hicho cha miaka miwili iwapo mlalamikaji atatoa sababu nzito sana za kuthibitisha kuwa anapata mateso makubwa.

### Kutengana

Kutengana sio talaka. Kutengana maana yake ni mume na mke kuishi mbalimbali. Kutengana kunaweza kuwa kwa mapatano kati ya mume na mke bila ya kufika mahakamani. Aidha kutengana kunaweza kutokana na amri ya mahakama kuwatenganisha wanandoa ikiwa mmoja wao atakuwa amepeleka ombi hili mahakamani.

### Kutengana kwa mapatano

Mume na mke kwa hiari yao wanaweza kukubaliana watengane ikiwa wameona hawaelewani katika maisha yao. Mapatano haya inashauriwa yawe ya maandishi. Mambo ya kuzingatia kwenye mapatano ni:-

i. Mume na mke wote wameridhia kuishi mbalimbali.
ii. Kutokubughudhiana, yaani hakuna ambaye atakwenda

kumbughudhi mwenziwe au kutaka kujamiiana naye.

iii. Mapatano ya matumizi kwa mke na watoto wa ndoa kama wapo.

iv. Mke kuishi maisha ya heshima.

v. Kama kuna watoto, mapatano yaeleze ni nani atakaa na watoto.

vi. Kama kuna mali ya pamoja, lazima kuwe na mapatano kuhusu usimamizi wa mali hiyo.

**Kutengana kwa amri ya Mahakama**

Sababu ambayo inaweza kuifanya Mahakama kutoa amri ya kutengana ni ile ile ya kuwa ndoa imevunjika. Ushahidi wa kuonyesha kuvunjika kwa ndoa ni ule ushahidi unaotakiwa katika talaka. Lakini mahakama inapotoa amri ya kutengana si lazima iamini kuwa ndoa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishwa. Mahakama ikishatoa amri ya kutengana inaweza pia kutoa amri mume ampe mke na watoto kama wapo kiasi fulani cha matumizi.

## SEHEMU YA PILI

**Sababu ya kutoa talaka**

Sababu pekee inayoipa mahakama kufikia uamuzi wa kutoa talaka ni baada ya kuridhika kuwa ndoa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishika tena.

Mambo yanayofanya ndoa ionekane kuwa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishika tena ni:-

**Ugoni**

Ugoni ni zinaa kati ya mwanamume na mwanamke ambao hawajaoana, ambapo mmojawapo au wote wana ndoa na kitendo hiki cha zinaa kiwe cha hiari.

**Ukatili**

Ukatili unakuwepo pale ambapo mlalamikaji ameumizwa mwili au kuharibiwa afya yake, au

kuwa na hofu ya kuamini kwamba hapo baadaye ataumizwa mwili au afya yake.



***Vipigo katika ndoa ni sehemu ya ukatili; hakuna mwanandoa anayeruhusiwa kumpiga mwenzake.***

**Kulawiti**

Kulawiti maana yake ni kumwingilia mtu kinyume na maumbile.

**Kichaa**

Ili talaka iweze kutolewa ni lazima madaktari wawili bingwa wa magonjwa ya akili wathibitishe kuwa ugonjwa huo hautapona.

**Kuzembea wajibu kwa makusudi**

Mume ana wajibu wa kumtunza mkewe, kwa kumpa chakula, mahali pa kulala na mavazi yanayofaa kulingana na hali yao ya maisha. Mke pia ana wajibu wa kumtunza mume ikiwa mke huyo anao uwezo na mume hawezi kujipatia pato lolote,kwa sababu ya maradhi au maumivu ya mwili.

Hivyo basi kama mume anaishi na mke, lakini hampi matumizi hata kidogo, au anatoa matumizi kidogo sana kwa mkewe ukilinganisha na uwezo wake na hali yao ya maisha,

huu unaweza kuwa ushahidi kuonesha kwamba ndoa imevunjika.

**Uasi (Utoro)**

Kuasi ni mume au mke kuhama kutoka nyumba ya ndoa na kwenda kuishi mahali pengine bila sababu yoyote na hadhamirii kurudi. Wakati mwingine mke huondoka kutokana na vitendo vya ukatili anavyofanyiwa na mume wake. Kisheria hapa mume ndiye aliyemwasi mke. Huu ndio unaoitwa "uasi wa hila". Kitendo cha uasi kikithibitika ni ushahidi wa kuonesha kuwa ndoa imevunjika.

**Kutengana**

Ikiwa mume na mke wametengana kwa muda usiopungua miaka 3, (au zaidi) kutengana kwao kutakuwa ni ushahidi kuonesha kwamba ndoa imevunjika.

**Kifungo**

Ikiwa mume au mke ametenda kosa la jinai na akafungwa kifungo cha maisha au kwa muda usiopungua miaka 5 talaka inaweza kutolewa kwa sababu hiyo.

**Dhana ya kifo**

Hii ni dhana kuwa mtu fulani huenda amefariki. Hali hii hutokea ikiwa mtu huyo ametoroka au kuondoka kwa siku nyingi na hajulikani alipo na juhudi za kupata habari zake hazikufanikiwa. Muda unaokubalika kisheria ni kuanzia miaka 5 au zaidi. Mahakama hutoa tangazo kuwa fulani inadhaniwa amefariki baada ya kuwasilishwa ombi mahakamani na mume au mke anayedhani kuwa mwenziwe huenda amefariki.

**Tofauti za Dini**

**Kubadilisha dini**

Iwapo mjibu maombi atabadili dini wakati wanandoa wote walikuwa wa dini moja wakati wa kufunga ndoa na iwapo kutokana na masharti ya dini ile kubadili dini kunavunja ndoa au ni sababu ya kuvunja ndoa, hii inaweza kuwa sababu kuwa

ndoa imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishwa tena.

## SEHEMU YA TATU

### Taratibu za kufuata wakati wa kuvunja ndoa

1. Mlalamikaji aende Baraza la Usuluhishi la ndoa linalotambuliwa kisheria Kama vile, BAKWATA, Kanisani au Baraza la Usuluhishi la kamishna wa Ustawi wa Jamii na Baraza la Kata.
2. Baraza la Usuluhishi likishindwa kusuluhisha, litatoa hati kuelezea maoni yake na kuelekeza shauri likatatuliwe Mahakamani.
3. Baada ya usuluhishi kushindikana mlalamikaji anapaswa aandike madai ya kuvunja ndoa na ayawasilishe Mahakamani akiambatanisha cheti cha ndoa kama kipo, hati ya Baraza la Usuluhishi wa ndoa iliyotolewa si zaidi ya miezi sita tangu siku ya kuwasilisha shauri hili mahakamani na hati yoyote ile ambayo angependa Mahakama ione ili kuimarisha ushahidi wake.

### Madai ya talaka yaoneshe yafuatayo:

- Kwamba kulikuwa na ndoa halali
- Kuna mgogoro kati ya wanandoa na jitihada za kusuluhisha zimefanyika lakini imeshindikana.
- Taja watoto wa ndoa, jinsi na umri wao (kama wapo).
- Taja mali mlizochuma wakati wa ndoa yenu.
- Mwisho aiombe mahakama itoe amri zifuatazo:-

  - Ndoa imevunjika na talaka itolewe.
  - Mgawanyo wa mali mlizochuma.
  - Mamlaka ya kuishi na watoto pamoja na matunzo yao iwapo unaona unahitaji na unaweza kuishi nao.
  - Mwenzi wako alipe gharama za kesi.

- Amri nyingine yoyote ambayo mahakama itaona inafaa.

Wasilisha madai haya mahakamani, utapewa namba ya kesi na utaelezwa siku ya kusikiliza kesi.

## SEHEMU YA NNE

### Mifano ya kesi za talaka zilizotolewa maamuzi mahakamani

Zifuatazo ni baadhi ya kesi zilizoamuriwa na Mahakama Kuu ya Tanzania na Mahakama ya Rufani Tanzania:

**Jalemela dhidi ya Shita (1970) H.C.D Na. 319**

**Maelezo**

Mke aliomba apewe talaka kwa sababu baada ya mume kuoa mke wa pili mume aliacha kabisa kulala na mke wa kwanza kwa muda wa miaka miwili. Baada ya kuona hivyo mke wa kwanza alihama kutoka nyumba yao ya ndoa na kwenda kuishi kwa wazazi wake.

Mahakama ya Mwanzo ilitoa talaka kwa mke kwa sababu mume ndiye aliyekuwa ni mwasi. Mume alipeleka rufani Mahakama ya Wilaya ambako rufani yake ilishindwa. Akapeleka rufani Mahakama Kuu ambayo pia iliunga mkono uamuzi wa Mahakama ya Mwanzo na ya Wilaya.

**Hukumu**

**Mnzavas Ag. J. alisema:**

"Mke alikata shauri kurudi kwa wazazi wake baada ya kuona kuwa mumewe hataki kulala nae kama mke kwa muda wa miaka miwili. Bwana hakuwa na sababu yoyote ya kufanya hivyo. Kwa hiyo ingawa mke ndiye aliyehama kimwili kutoka nyumba ya ndoa, lakini kwa maoni yangu naona mume hasa ndiye aliyemwasi mke kwa hila. Kwa hiyo mke alikuwa na haki ya kupewa talaka".

## Hall dhidi ya Hall (1962) 1 W.L.R. 1246

### Malezo

Kesi hii ilitokea huko Uingereza. Mume alikuwa anakunywa na kulewa pombe mara kwa mara na kurudi nyumbani usiku wa manane na wakati mwingine alfajiri. Kila alipokuwa anarudi alipiga kelele na kumwamsha mke na watoto usingizini. Mke alishindwa kuvumilia tabia hiyo, hivyo aliondoka na kumwacha mume peke yake, kisha alifungua madai kwamba mume ndiye aliyemwasi.

### Hukumu

Hakuna shaka yoyote kwamba mke aliona hawezi kuendelea kuishi katika hali ya namna hii. Inawezekana kwamba mume alikuwa hana nia ya kutaka mkewe aondoke alipokuwa anafanya mambo yake ya ulevi. Lakini ilimpasa kujua kwamba mke asingeweza kuendelea kuishi katika hali kama hii kwa muda mrefu zaidi. Mume ndiye aliyemwasi mke.

## Fatu Musa dhidi ya Rashidi Makhame (1975) TLR Na. 10

Mke alikuwa ameishi na mumewe kwa muda usiopungua miaka 20. Baadaye mume alipatwa na ugonjwa wa ukoma na kwenda kutibiwa hospitali kwa muda mrefu. Baada ya kupona alirudi nyumbani, lakini alikuwa akienda hospitali mara kwa mara kutibiwa.

Baada ya mume kurudi hospitali mke alifungua madai ya talaka kutaka kuachana na mumewe. Sababu aliyoitoa ni kwamba mumewe ana ukoma. Mahakama ya Mwanzo ilikataa kutoa talaka. Mke aliomba rufani na hata kesi ilifika Mahakama Kuu.

### Hukumu

**Kisanga, J. alisema**

Kifungu 107(2) cha Sheria ya Ndoa, 1971 kimeorodhesha sababu ambazo ni ushahidi kuonesha kuwa ndoa imevunjika. Ila katika orodha

hiyo ukoma si mojawapo. Licha ya hivyo, kuruhusu kutoa talaka katika hali kama hii ni kutoa mfano mbaya kwa waume kuwaacha wake zao, au wake kuwaacha waume zao kwa sababu ya ugonjwa. Kufanya hivyo ni kuingiza udhaifu katika ndoa".

**Ester Mponda dhidi ya Bakari Nahoda (1982) TLR 202**

**Maelezo**

Mke na mume walikuwa wameishi kwa muda wa miaka 8. Mke alipeleka shauri la madai ya talaka kwa sababu mume alikuwa hampi uhuru wa kutumia kipato alichokuwa anachuma mwenyewe.

**Hukumu**

Mahakama ilikataa kutoa talaka kwa kuwa sababu iliyotolewa siyo nzito na mahusiano kwenye ndoa yalikuwa hayajavunjika kiasi ambacho hayawezi kurekebishwa.

**Mambo ya kuzingatia**

- Endapo mume atafanya vitendo vibaya ambavyo vitamsababisha mkewe aondoke kwenye nyumba ya ndoa, mume ndiye anayehesabika kuwa amemwasi mkewe kwa hila; Ijapokuwa mke ndiye aliyeondoka katika nyumba ya ndoa.
- Mume au mke anaweza kuhesabika kuwa amemwasi mwenzie hata kama wanaishi kwenye nyumba moja na hata chumba kimoja kama mume au mke atakuwa amekataa kushiriki tendo la ndoa kwa muda mrefu bila sababu yoyote.
- Mume au mke akimruhusu mwenzie kuzini hawezi baadae kudai talaka akitumia uzinifu wa mkewe au mumewe kwa sababu aliruhusu zinaa hiyo.
- Mahakama haiwezi kumpa mume au mke talaka kwa sababu mwenziwe

amepatwa na ugonjwa unaotibika na wa kawaida.

- Mahakama inaweza kubadilisha mapatano yoyote kuhusu matumizi ya mke baada ya kutengana au kutoa talaka kama kuna lazima ya kufanya hivyo.

## MASWALI

1. Talaka ni nini? Kabla ya kutoa talaka Mahakama huangalia mambo gani?
2. Kuna aina ngapi za kutengana? Zitaje na uzifafanue.
3. Bwana Makeke amekuja kwako kuomba ushauri. Anataka kumuacha mkewe kwa sababu amezaa watoto wa kike tu - Utamshauri nini?
4. Taja taratibu za kufuata kabla ya kuvunja ndoa.

# SURA YA NNE

# HAKI ZA MTOTO

## UTANGULIZI

Watoto ni sehemu ya jamii na wanahitaji uangalizi wa jamii nzima. Hivyo; kutokana na kuwepo kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za watoto hapa nchini, sura hii itasaidia kuelimisha jamii umuhimu wa kuzilinda haki za watoto na kuchukua hatua za kisheria pale haki hizo zinapovunjwa.

Haki za watoto zina umuhimu mkubwa na zinatakiwa kuzingatiwa kwa makini zaidi hivi sasa, kutokana na janga la UKIMWI ambalo linaendelea kuangamiza nguvu kazi ya Tanzania. kumekuwepo na matukio mbalimbali ya maambukizi ya makusudi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa watoto na vijana wadogo. Hivyo basi, ni muhimu jamii kuacha tabia ya kuambukiza watoto VVU kwa makusudi kwani kwa kufanya hivyo tunaangamiza taifa la kesho.

## Mtoto ni nani?

Hili ni swali muhimu katika maelezo yote ya sura hii. Ni vizuri tufahamu mtoto anavyofahamika kisheria kwa sababu mtu yeyote anaweza kuwa mtoto kulingana na tafsiri tofauti zilizopo. Kamusi ya Kiswahili inamweleza mtoto kuwa ni:

(a) Mwanadamu au mnyama ambaye hajakaomaa.

(b) Jina analoitwa kiumbe ambaye amezaliwa na wazazi wake wawili.

Kwa tafsiri ya pili sote tu watoto bila kujali umri au maumbile.

## Kisheria Mtoto ni Mwanadamu yeyote mwenye Umri chini ya Miaka Kumi na Minane

Katika kitabu hiki tutakapozungumzia mtoto ni kwa mujibu wa tafsiri ya kisheria. Mtu yeyote aliye zaidi

ya miaka kumi na nane si mtoto tunayemzungumzia hata kama bado anategemea wazazi wake.

**Kwa nini Haki za Mtoto**

Haki ni hali ya kustahili jambo. Mtoto kama binadamu ana mambo muhimu anayostahili ili aweze kuishi, kukua na kuendelea. Kama tasfiri ya mtoto ilivyo ni kweli kwamba mtoto;

- Anategemea kwa kiasi kikubwa sana walezi wake ili apate stahili zake zote.
- Hata pale anapojaribu kupata stahili hizo binafsi bado anapaswa kusaidiwa ili asidhurike kwa hali yoyote.
- Asipopatiwa stahili zake anaweza kupoteza uhai wake, au makuzi yake yakawa potofu.

Hivyo ni sahihi kabisa kusema haki za mtoto ni muhimu kwa kuendeleza jamii. Watoto wakitunziwa haki; jamii inahakikishiwa kuendelea. Mtoto akikosewa haki kuna uwezekano mkubwa wa jamii kutoendelea. Pengine jamii iliyokosea watoto wake haki zao itajijengea msingi mbaya kwa kuwa na jamii yenye watu wasioelimika au magoigoi kulingana na haki ipi mtoto amekosewa.

**Hadhi ya Mtoto**

Mtoto kama tulivyomweleza kisheria ana hadhi yake. Kwa ujumla watoto wamegawanyika kutokana na hadhi walizonazo kisheria. Wapo watoto wanaoitwa halali na watoto




wasio halali. Watoto halali ni wale waliozaliwa wazazi wao wakiwa na ndoa au waliohalalishwa kwa wazazi

wao kufunga ndoa baada ya kuwazaa watoto hao. Watoto wasio halali ni wale waliozaliwa wazazi wao wakiwa hawana ndoa na wakabaki vivyo hivyo. Mara nyingi watoto hawa huitwa watoto wa nje ya ndoa.

**Zingatia kuwa**

Watoto wote bila kujali hadhi hizo hapo juu wana haki sawasawa. Hivyo mtoto awe wa halali au asiye halali anastahili haki zote kama mtoto. Tofauti ni kuwa sheria na mazingira ya kupata baadhi ya haki hizi ni tofauti. Zipo sheria zinazolenga kulinda haki za mtoto wa halali katika baadhi ya haki na zipo sheria zinazolenga kulinda haki za mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa.

Watoto kwa kuwa ni binadamu wanastahili haki zote sawasawa, wawe weupe, weusi, wa kike au wa kiume, waislamu au wakristo, halali au wasio halali. Haki za mtoto ni kwa watoto wote.

## SEHEMU YA KWANZA

### Haki za Mtoto Kimataifa

Jumuiya ya kimataifa imelipa kipaumbele suala la haki za watoto kwa kupitisha mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto. Mkataba huu wa kimaitaifa umepitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1989 kufuatia tamko la haki za mtoto la mwaka 1959. mkataba huu ulianza kutumika rasmi mwaka 1990 baada ya nchi zaidi ya ishirini kuuridhia.

### Mkataba huu una Umuhimu gani Tanzania

Tanzania ilitia saini Mkataba wa Haki za Mtoto mwaka 1990 na ikauridhia mwaka 1991. Nchi inaporidhia mkataba inawajibika kutekeleza kikamilifu yote yaliyo ndani ya mkataba. Kwa mujibu wa sheria za mikataba ya kimataifa mkataba ulioridhiwa unapaswa uwe sehemu ya sheria za nchi iliyouridhia. Kwa mantiki hii basi, mkataba huu ni sehemu au unapaswa kuwa sehemu ya

sheria za Tanzania. Tanzania inatakiwa ihakikishe watoto wake wanafaidi haki zote zilizotajwa ndani ya mkataba huu wa haki za mtoto.

**Haki zilizotajwa katika Mkataba wa Haki za Mtoto**

Mkataba huu umefafanua haki za mtoto kuwa ni haki ya **kuishi, kulindwa, kuendelezwa na kushiriki.**

Imeelezwa kuwa mtoto kwa sababu za kutopevuka kimwili na kiakili, anahitaji malezi maalumu na kulindwa, vikijumuisha ulinzi unaofaa kisheria kabla na baada ya kuzaliwa. Kwa mujibu wa mkataba huu mtoto ni kila binadamu mwenye umri chini ya miaka 18 labda, chini ya sheria inayotumika kwa mtoto huyo, umri wa utu uzima uwe umefikiwa mapema.

**Haki za Mtoto zilizoainishwa katika Mkataba**

- Kila mtoto ana haki ya asili ya kuishi, kusajiliwa na kupewa jina mara tu anapozaliwa.
- Kuishi na wazazi wake mradi hali hii ionekane inalingana na maslahi makuu ya mtoto.
- Kudumisha mawasiliano na wazazi wake wote wawili kama wazazi hao wametengana/wameachana
- Kupata kwa kiwango kikubwa matunzo ya afya na tiba.
- Kupatiwa elimu. Nchi iliyotia saini mkataba ihakikishe inatoa elimu ya msingi bure na elimu hiyo iwe ni ya lazima kwa wote.
- Kunufaika na usalama wa jamii ikiwa ni pamoja na hifadhi.
- Kukutana na wengine na kujiunga au kuunda vyama.
- Kutoa maoni yake bila hofu na maoni hayo yazingatiwe katika suala lolote au utaratibu unaomwathiri.
- Kupata taarifa, kuyafanya mawazo na taarifa zifahamike, bila kujali mipaka. Nchi ihakikishe

kuwa mtoto anapata taarifa na habari kutoka vyanzo mbalimbali na taarifa hizo ziwe na manufaa kwa mtoto kijamii na kiutamaduni.

- Kulindwa dhidi ya dhuluma na kupuuzwa na aina nyingine zozote za ukandamizaji.
- Kulindwa dhidi ya kufanyishwa kazi itakayoathiri afya, elimu au maendeleo yake.




- Kulindwa dhidi ya matumizi ya madawa ya kulevya.
- Kulindwa dhidi ya ukandamizwaji wa kijinsia na kutumiwa vibaya ikiwa ni pamoja na kuingizwa kwenye umalaya na kuhusishwa na maonesho ya uchi.
- Kushirikishwa katika mapumziko, burudani na shughuli za utamaduni.

**Watoto wenye ulemavu**

watoto wenye ulemavu wana haki ya kupata matunzo maalum, elimu na mafunzo kuwasaidia wanufaike kikamilifu na kuishi maisha ya heshima ya utu na kufikia kujitegemea kwa kiwango kikubwa iwezekanavyo.

**Watoto wakimbizi**

Watoto wakimbizi au watoto wanaotafuta hadhi ya ukimbizi wana haki ya kupatiwa hifadhi maalum. Nchi ikishirikiana na mashirika yanayohusika na hifadhi hiyo ihakikishe watoto wakimbizi wanahifadhiwa.

**Watoto walioathirika na mambo mbalimbali**

Watoto walioathirika na migogoro ya kijeshi, mateso au

kutopatiwa matunzo, kutendwa vibaya au kukandamizwa wana haki ya kushughulikiwa vyema ili wahusishwe na kurejeshwa kwenye jamii.

**Watoto walio katika mgongano na sheria**

Watoto wanaokiuka sheria wana haki ya kuendeleza hali ya utoto; kujiona wana hadhi na thamani. Watoto hawa wana haki ya kupatiwa uhakikisho wa msingi pamoja na msaada mwingine kwa ajili ya kujitetea.

**Muhimu**

**Nchi zilizouridhia Mkataba huu zinapaswa**

- Kufanya lolote linalowezekana kutekeleza haki zilizomo kwenye Mkataba huu.
- Kuzingatia kikamilifu maslahi makuu ya mtoto katika hatua zote zinazomhusu mtoto.
- Kuhakikisha haki zilizomo kwenye Mikataba zinajulikana kwa mapana sana miongoni mwa watu wazima na watoto.

**Mkataba wa Afrika juu ya Haki na Maslahi ya Mtoto.**

Mkataba huu ulipitishwa na kutiwa saini na nchi za Afrika mwezi Julai 1990. Mkataba huu unashughulikia baadhi ya masuala ambayo ni mahsusi kwa mtoto wa Afrika, kwa mfano wajibu wa mtoto na nafasi yake katika ukoo/familia.

Mkataba huu unatambua kuwa mtoto anashika nafasi ya pekee na ya muhimu katika jamii ya kiafrika na kuwa mtoto anastahili kukua katika mazingira ya familia.

Mkataba pia unatambua kwamba katika mambo yote yanayofanywa na mtu au mamlaka yoyote kumhusu mtoto, maslahi bora ya mtoto itakuwa ndio suala la msingi kuzingatiwa.

**Swali**

**Unapofundisha somo hili waulize washiriki maswali haya ya changamoto**

1. Je wewe kama Mtanzania umewahi kabla ya kusoma hapa kufahamu juu ya Mikataba hii miwili juu ya haki ya mtoto?

2. Je unafikiri kuna umuhimu kwa watoto kufahamu mikataba hii?

3. Toa pendekezo namna mikataba hii inavyoweza kufahamika kwa watoto na watu wazima.

## SEHEMU YA PILI

### Haki za Mtoto Tanzania

Watoto wa Tanzania kama watoto wa ulimwengu wote wanapaswa kupewa haki wanazostahili. Hivyo tutaangalia jinsi Tanzania ikiwa nchi iliyotia saini mkataba wa haki za Mtoto, inavyompatia mtoto wa Kitanzania haki zake. Tutaangalia sheria za nchi zinazolenga kumpatia mtoto haki zake. Kuhusu hali halisi ya utekelezwaji wa sheria hizo mnaweza kuangalia katika mazingira yenu iwapo kweli watoto wanapatiwa haki hizo au la.

### Sera ya Haki za Mtoto

Sera ni muongozo au miongozo inayoeleza kwa ujumla mambo fulani fulani yanavyopaswa kuwa. Mfano Sera ya Elimu inatoa muongozo juu ya elimu itolewe vipi, wapi na nani na ya aina gani. Hivyo kwenye suala la Haki za mtoto ni muhimu kuwepo Sera. Chama cha Mapinduzi (CCM) kilitoa Sera ya Malezi ya Taifa kwa Watoto na Vijana Tanzania mwaka 1987. Haki za mtoto Tanzania zinapatikana katika sheria mbalimbali zinazogusa haki hizo.

### Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971

Sheria hii ina vipengele kadhaa vinavyompa mtoto haki. Sheria

hii inawahusu watoto wale tu waliozaliwa kwenye ndoa au waliohalalishwa na ndoa. Kwa mujibu wa sheria hii ni wajibu wa mwanaume/baba kutunza watoto wake kwa kuwapatia mahitaji yao muhimu.Wajibu huu unapaswa kutimizwa na mwanaume huyu hata kama haishi na wanawe. Wajibu huu utamrudia mama wa watoto iwapo imethibitika kisheria kuwa baba yao hana uwezo hajimudu, au amepotea kwa muda mrefu na hajulikani aliko au amefariki.

Kukosa kumpatia mtoto haki hizo ni kosa la jinai. Katika sheria hii pia inaelezwa kuwa iwapo wazazi watatengana au kuachana, watoto wataishi pale ambapo ustawi na makuzi yao bora yatapewa uzito. Sheria hii inatamka pia kuwa ni vema mtoto wa umri chini ya miaka saba kuishi na mama yake kwa maslahi makuu ya mtoto.

Mahakama inaweza kumwamuru baba wa watoto kutoa matunzo kwa watoto wake pale inapothibitika kuwa ameitelekeza familia au amedharau kutoa matunzo bila sababu ya msingi.

Mtu anaweza kuoa au kuolewa akifikia umri wa miaka 18. Ila msichana anaweza kuolewa akiwa na umri chini ya miaka 18 kwa idhini ya mzazi lakini umri huo usiwe chini ya miaka 15. Mvulana anaweza kuoa chini ya miaka 18 lakini si chini ya miaka 16 kwa idhini ya wazazi. Watoto wa umri usiopungua miaka 14 wa kike wanaweza kuolewa kwa idhini ya Mahakama.

**MUHIMU**

*Kutengana, talaka na migogoro katika familia ni chanzo kikubwa kinachoathiri maendeleo ya mtoto kielimu, kiafya na kisaikolojia. Pale familia inaposambaratika, watoto hupoteza mwelekeo na kuanza kuishi katika familia mpya ama kuhama kutoka kwa mlezi mmoja hadi mwingine.*

*Uhamaji huu huharibu maendeleo ya mtoto na mtiririko mzima wa kukua kwake kimaadili. Mwisho wa siku mtoto huishia mtaani akikwepa adha anazozipata toka kwa mzazi/mlezi mmoja hadi mwingine.*

**Swali**

1) Unafikiri kuna sababu zozote za msingi za kuruhusu watoto wadogo kuoa au kuolewa? Je kuna sababu za kubagua wasichana na wavulana?

2) Kanuni za afya zinasemaje juu ya mtoto wa umri mdogo kuzaa?

**Sheria ya Matunzo kwa Watoto Waliozaliwa Nje ya Ndoa**

Sheria hii imetungwa kulinda haki za watoto waliozaliwa nje ya ndoa. Ni sheria inayohusu matunzo na elimu ya watoto hawa. Watoto waliozaliwa nje ya ndoa huitwa watoto wa ujombani. Watoto hawa wana haki pia ya kulelewa. Mwanamke anayepata mtoto nje ya ndoa anastahili kupatiwa matunzo ya mtoto wake toka kwa aliyetangazwa kisheria baba mhusika wa mtoto. Matunzo kwa Watoto waliozaliwa nje ya ndoa, yatatolewa endapo mama wa mtoto ataithibitishia mahakama kuwa mwanaume anayetajwa ndiye mhusika wa mototo.

**(i) Amri ya matunzo**

Mwanamke aliyepata ujauzito nje ya ndoa anaweza kuomba Mahakama ya Wilaya kutoa amri ili baba wa mtoto atoe fedha za matunzo kwa ajili yake wakati wa ujauzito na kwa ajili ya mtoto baada ya kujifungua. Mahitaji ya mtoto ni yale ya kawaida yaani chakula, malazi mavazi, elimu na matibabu.

**(ii) Muda wa kupeleka maombi ya matunzo ya mtoto mahakamani**

- Maombi ya matunzo ya mtoto yapelekwe katika

mahakama ya wilaya ile ambapo anayedhaniwa baba wa mtoto huyo aidha anafanya kazi, au anaishi. Maombi haya ni lazima yawasilishwe mahakamani ndani ya miezi 12 tangu mtoto huyo alipozaliwa.

- Kama baba wa mtoto aliondoka nchini basi atakaporudi, maombi ya matunzo yapelekwe katika Mahakama ya wilaya ndani ya miezi 12 tangu baba wa mtoto aliporejea nchini.
- Kama baba wa mtoto alikuwa anatoa matuzo na baadaye akaacha, basi maombi ya matunzo yapelekwe ndani ya miezi 12 tangu baba wa mtoto alipoacha kutoa matunzo.

Mahakama haitakubali maombi ya matunzo mpaka imeridhika kuwa kuna sababu za kuamini kuwa:-

- Aliyetajwa kuwa baba wa mtoto, ni kweli baba wa mtoto huyo.
- Mama wa mtoto amemtaja baba huyo kwa nia njema, si kwa kutaka kumwaibisha au kumfanyia vitimbi.
- Baba huyo ametakiwa kumtunza na kumpatia matunzo mtoto na amekataa au kupuuza kufanya hivyo au hakufanya kwa ukamilifu.

Mahakama ikiridhika kutokana na maelezo ya mama wa mtoto huyo na ikithibitishwa kwa ushahidi mwingine kuwa aliyetajwa ndiye baba mhusika wa mtoto, basi mahakama itatoa tamko kwamba yeye ndiye baba mhusika wa mtoto. Mahakama itatoa amri ya kumtaka baba huyo kumlipa mama wa mtoto au mtu anayemtunza mtoto huyo kiasi cha fedha kisichozidi shilingi 100/- kwa mwezi kama fedha ya matunzo, matibabu na elimu ya mtoto. Au, mahakama inaweza kutoa amri ya malipo ya mkupuo yasiyozidi shilingi 15,000/- ambazo zitalipwa mahakamani na kutumika

katika kumtunza huyo mtoto na kulipa gharama za elimu yake.

### (iii) Kukoma Kwa Matunzo

Sheria imeweka mazingira ambayo baba mhusika atasitisha matunzo ya mtoto. Mazingira haya ni:

- Pale ambapo mtoto atatimiza umri wa miaka 16.
- Pale ambapo mama wa mtoto huyo ataolewa.
- Baba wa mtoto huyo anapofariki.
- Mahakama ikipewa sababu za kuridhisha matunzo yatasitishwa mtoto akiwa na umri wa miaka 14.

### (iv) Upungufu katika Sheria ya Matunzo kwa Watoto Waliozaliwa Nje ya Ndoa.

- Kiasi cha shilingi 100/- kwa mwezi au shilingi 15,000/- kwa mkupuo ni kidogo sana kutokana na hali halisi ya mahitaji ya mtoto kwa wakati huu.
- Kusitishwa matunzo wakati mama wa mtoto anapoolewa inaweza kumuathiri mtoto, hasa ikiwa mama atolewa na mwanaume mwingine na ikabidi mtoto akaishi kwa bibi au mtu mwingine.
- Kusitishwa matunzo mtoto afikapo umri wa miaka 16 au 14 ni kinyume cha tafsiri ya mtoto ambaye ni yule wa chini ya umri wa miaka 18. Mara nyingi watoto wa umri wa miaka 14 na 16 huwa bado wako shuleni na mahitaji yao ni mengi zaidi.
- Adhabu ya kosa la kushindwa kutoa matunzo ni kifungo cha miezi mitatu. Adhabu hii ni ndogo sana kulingana na kosa lenyewe kwani mtoto anakosewa haki kwa kiasi kikubwa.

**Swali**

Jadili mapungufu ya sheria hii na toa mapendekezo ya kurekebisha mapungufu hayo.

**Sheria ya Elimu ya mwaka 1978**

Sheria hii imetafsiriwa na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Wizara ya Elimu na Utamaduni (ya 1995) inataka kila mtoto aliyetimiza miaka saba ajiunge na shule ya Msingi. Ni lazima mtoto aandikishwe na kuhudhuria shule. Elimu inamsaidia mtoto kukua kwa ukamilifu na kuelewa mazingira yanayomzunguka. Sheria inaeleza wazi kuwa elimu ya msingi ni ya lazima kwa watoto wote na itatolewa bure. Kanuni zinazohusika na sheria hii zinahesabu kuwa ni kosa kwa mzazi atakayeacha kumwandikisha shule mtoto mwenye umri wa kwenda shule. Umri wa kwenda shule. Vile vile ni kosa kwa mzazi kutohakikisha kuwa mtoto wake anaendelea na masomo hadi kufikia darasa la saba. Mtu yeyote atakayesababisha mtoto asiendelee na shule naye pia atatiwa hatiani. Ifahamike pia kuwa chini ya kanuni hizi utoro ni kosa la jinai. Hivyo basi mtoto mtoro au mzazi ambaye anasababisha mtoto wake awe mtoro wote wanaweza kushitakiwa kwa kosa la jinai.

**Swali**

- Je sheria hii inatekelezwa vipi katika sehemu mnayoishi?

**Sheria ya Elimu 1978 (Tangazo la serikali Na: 265/2003)**

[Kanuni ya Elimu ya kutoa adhabu kwa watu wanaooa au kuwapa ujauzito wanafunzi]

Kutokana na kuongezeka kwa matukio ya wasichana kuachishwa masomo kwa ajili ya kuozwa au kupewa ujauzito, Wizara ya Elimu ilitoa kanuni zinazolenga matatizo haya kwa wasichana wa shule za msingi na sekondari. Kanuni hizi zimeainisha majukumu na adhabu pale matendo haya yanapofanywa. Chini ya kanuni hizi;

- Kila Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu anawajibika kuhakikisha kuwa kila msichana aliyedahiliwa katika shule yoyote anahudhuria hadi kumaliza muda wa masomo uliopangwa na kukamilisha elimu ya kiwango alichodahiliwa.

- Mzazi yeyote anayesaidia, kufumbia macho au kushawishi msichana wa shule kuolewa wakati anasoma elimu ya msingi au sekondari atakuwa ametenda kosa na adhabu yake ni faini isiyozidi shilingi 100,000/- au kifungo kisichozidi miaka 2 au vyote kwa pamoja.

- Mtu yeyote ambaye katika mazingira yoyote atamuoa msichana anayesoma shule anatenda kosa na adhabu yake ni faini kati ya shilingi 300,000/- hadi 500,000/- au kifungo kisichozidi miaka 3 au vyote.

- Mwanaume yeyote atakayempa ujauzito msichana anayesoma anatenda kosa na adhabu ni kifungo cha kati ya miaka 3 hadi 6 bila mbadala wa faini.

- Katika kuanzisha mashtaka dhidi ya wanaooa au kuwapa ujauzito wanafunzi, Afisa Elimu wa Wilaya atahusika kwa shule za msingi na Afisa Elimu wa Mkoa atahusika na shule za sekondari. Pamoja na hawa mtu yeyote anaweza kuanzisha mashtaka dhidi ya watu hawa.

- Kila Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu ataweka kwa umakini kumbukumbu na kuzituma kila baada ya robo ya mwaka kwa kamishna wa Elimu au mwakilishi wake ripoti ya kina juu ya matukio ya ujauzito na kuolewa wanafunzi na

hatua zilizochukuliwa dhidi y a wakosaji.

- Iwapo mwanafunzi atakuwa amebakwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana Na. 4 ya 1998 itatumika.

**Kuandikisha Watoto shule**

Sheria ya Serikali za Mitaa (Tawala za Wilaya) ya mwaka 1982 Sura ya 287 kama sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002 imezipa mamlaka za Wilaya uwezo wa kuhakikisha kuwa mtoto anaandikishwa shule ya msingi. Sheria hii pia imeunda kamati za kupita mashuleni na kuhakikisha kuwa watoto wameandikishwa shule na wanahudhuria masomo.

**Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi ya mwaka 2004**

Sheria hii inamlinda mtoto dhidi ya ajira ngumu zisizolingana na umri wake. Sheria inaharamisha ajira ya watoto



chini ya umri wa miaka 14. Na kama watoto wenye zaidi ya miaka 14 wataajiriwa, lazima muajiri ahakikishe watoto hao wanakwenda shule. Vilevile watoto chini ya miaka 18 hawaruhusiwi kufanya kazi kwenye migodi, viwanda, ukuli, kwenye meli au kwenye maeneo ya kilimo ambayo si salama na kwenye baa.

***Hali Halisi***

*Pamoja na Sheria ya Ajira kukataza ajira ya watoto, watu wengi wameajiri watoto na kuwafanyisha kazi za ndani kwa ujira mdogo. Wafanyakazi wa ndani ambao ni watoto hunyanyaswa na kufanyiwa vitendo viovu kinyume na haki*

*za msingi za mtoto. Migodi mingi na mashamba makubwa ya chai na kahawa yameajiri watoto kwani ajira ya watu wazima ni gharama. Ni wajibu wetu kuhakikisha ajira za hatari kwa watoto zinatokomezwa.*

**Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo Sura ya 13**

Sheria hii inataja haki za watoto wa mitaani. Ni wajibu wa Afisa Ustawi wa Jamii au Polisi kuwachukua watoto wanaonekana mitaani bila shughuli maalum. Baada ya kuwachukua watoto hawa wanapaswa kuwahifadhi kwa nia ya kuwarejesha kwa wazazi au walezi wao.

Pia Sheria inatoa ulinzi kwa watoto watukutu na inatamka kwamba kesi za watoto ziwe zinasikilizwa faragha na zisiandikwe kwenye vyombo vya habari. Kama Kesi hizo zitatolewa taarifa kwenye vyombo vya habari, basi jina la mtoto lisitajwe. Sababu kubwa ni kumlinda mtoto na aibu ya kubezwa na kutokukubalika tena katika jamii inayomzunguka.

Kesi ya mtoto inapopelekwa ama kusikilizwa na mahakama, basi hakimu, wakili na polisi lazima wavae kiraia ili kumtoa mtoto hofu ya kuongea.

Sheria hii pia inawalinda watoto wanaopatikana na hatia na kuipa jukumu serikali kutafuta vyanzo vya matatizo na kuwarekebisha watoto hao badala ya kuwafunga. Na kama watoto hao watahukumiwa kifungo basi watatakiwa wapelekwe kwenye shule maalum za kuwarekebisha (approved schools). Bahati mbaya, hapa Tanzania shule hizo ziko tano tu na hazitoshelezi. Kutokana na uhaba wa shule hizo watoto hao huchanganywa kwenye jela za watu wazima kinyume cha sheria. Hali hii huwaathiri watoto kwani wengi hulawitiwa na kuambukizwa magonjwa ya

zinaa pamoja na virusi vya UKIMWI.

Sheria inakataza kuchanganya wafungwa watu wazima na watoto wanapokuwa gerezani. Serikali na jamii haina budi kutenga fungu la kujenga mahabusu na shule za watoto na kulinda watoto dhidi ya ukatili na magonjwa wanayoweza kuambukizwa wakiwa gerezani.

**Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16 (Penal Code)**

Sheria hii ina vifungu mbalimbali vinavyolinda haki za mtoto. Imetaja makosa ambayo mtu akipatikana na hatia huadhibiwa, nayo ni:-

- Kumnyima mtoto mahitaji yake muhimu, kama chakula, malazi n.k.
- Kutoa mimba au kusababisha mimba itoke.
- Kusababisha mtoto asizaliwe hai kwa uzembe.
- Kudhuru maisha ya mtoto aliyezaliwa.
- Wizi wa watoto
- Kumuonea kwa kumpiga au kumuumiza mtoto.
- Kumnajisi mtoto
- Kumzini mtoto wa kike mwenye umri chini ya miaka 18
- Kumsababisha mtoto asiendelee na masomo, mfano, kumpa mimba.
- Kumbaka mtoto
- Kumshirikisha mtoto kwenye vitendo viovu, kama wizi, mauaji n.k.
- Kumpa mimba mtoto wa shule.
- Sheria hii pia inatoa adhabu kwa wale wanaowaweka watoto katika mazingira ya hatari ambayo yanaweza kusababisha madhara kwa mtoto.

Sheria hii imejaribu kumlinda mtoto dhidi ya kuonewa na kunyanyaswa lakini haikukabili mambo yote muhimu.

Hivi karibuni imepitishwa sheria ambayo imerekebisha sheria hiyo pamoja na sheria zingine,

nayo inaitwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998.

**Sheria ya Mazao ya Tumbaku ya mwaka 2003**

Sheria hii ina vipengele ambavyo ni mahususi kwa ajili ya kumlinda mtoto. Pamoja na kuwa haikumtaja mtoto ni nani lakini inalenga kumlinda mtu ambaye katika ulingo wa harakati za kutetea haki za mtoto anayelindwa ni mtoto kwani inamlenga mtu mwenye umri chini ya miaka 18.

Kinga dhidi ya mtoto kutumia au kupewa tumbaku

- Lengo la kwanza la kisera la sheria ni kupunguza matumizi ya tumbaku na madhara yanayoambatana nayo kwa kuwalinda walio na umri chini ya miaka 18 na wengine wasiovuta tumbaku na mazao yake wasishawishike kutumia mazao ya tumbaku.

- Sheria hii imekataza yafuatayo;

  ✓ Hakuna mtu mwenye umri chini ya miaka 18 anaruhusiwa kuvuta au kuuza, kukopesha, kutoa au kumpa mtu tumbaku au mazao yake.

  ✓ Hakuna mtu anayeruhusiwa kumuuzia, kumkopesha au kumpa tumbaku mtu mwenye umri chini ya miaka 18 mahali popote.

Ni kinga kwa mtu iwapo atathibitisha kama hakujua aliyempa tumbaku na mazao yake alikuwa na umri zaidi ya miaka 18. Vilevile inaweza ikawa kinga iwapo mtu mwenye chini ya miaka 18 iwapo anafanya au kuhusiana na shamba au duka la familia.

**Maeneo yanayokatazwa kuuzia tumbaku na mazao yake.**

Katika kuuza tumbaku na mazao yake imekatazwa kuwa;

- Hairuhusiwi kuuza tumbaku na mazao yake katika maeneo au majengo yanayotumika kutoa elimu ya msingi na sekondari.
- Kuuza tumbaku na mazao yake katika maeneo au ndani ya kituo cha watoto.
- Kuuza tumbaku na mazao yake katika maeneo ya umma au maeneo yaliyotengwa maalumu kwa ajili ya watu wenye umri chini ya miaka 18.

**Kinga dhidi ya kuwatumia watoto kwenye matangazo ya biashara.**

Katika kufanya matangazo ya biashara ya tumbuku na mazao yake hairuhusiwi;

- Kufanyia matangazo hayo kwenye eneo linalotoa elimu.
- Hakuna mtu au chombo kinachoruhusiwa kumtumia mtu mwenye umri chini ya miaka 18 katika shughuli ya kutangaza biashara au tukio lolote lililodhaminiwa na kiwanda cha tumbaku.

Sheria imetamka bayana kuwa mtu yeyote katika kuendesha biashara zake akimpa bure mtu mwenye umri chini ya miaka 18 tumbaku, mazao ya tumbaku au nembo yoyote inayohusiana na tumbaku anatenda kosa na adhabu yake ni faini ya shilingi 500,000/- au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote.

**Zuio la watoto kupewa bidhaa zinazotangaza tumbaku na mazao yake.**

- Katika kufadhili matangazo ya kuhamasisha matumizi ya tumbaku na mazao yake.

  - ✓ Hairuhusiwi kufadhili Kwa namna yoyote kitu chenye uhusiano na kutangaza biashara ya mazao ya tumbaku, aina za mazao ya tumbaku, au mzalishaji wa mazao ya tumbaku

vinavyowahusu watu walio chini ya miaka 18.

- ✓ Aliye na umri chini ya miaka 18 haruhusiwi kuvaa tangazo, nembo au jina la zao la tumbaku katika mchezo, au shughuli au tukio lolote.
- ✓ Hairuhusiwi mtu yeyote kutoa kitu, nguo au kitu chochote cha kuuza au bure chenye jina, alama au nembo ya bidhaa ya tumbaku katika michezo ya kutangaza biashara kwa mtu mwenye umri chini ya miaka 18.

**Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya 1989**

Sheria hii ilianza kutumika tarehe 1 Julai 1998. Sheria hii inamlinda mtoto dhidi ya kudhalilishwa kwa makosa mbalimbali ya jinai. Sheria kama hii pia imepitishwa kule Zanzibar.

Madhumuni ya sheria hii ni kuingiza katika baadhi ya sheria, masharti maalum kisheria kuhusiana na makosa hayo ya kujamiiana au yanayowahusu watoto. Nia ni kuimarisha azma ya taifa ya kuhifadhi stahili za watoto na wanawake kuhusiana na haki binafsi za kuishi, heshima na uhuru. Mtoto analindwa na sheria hii katika vifungu vilivyorekebisha Sheria zipatazo tano ikiwemo Sheria ya Kanuni za Adhabu na katika vifungu vipya vilivyowekwa, mambo yafuatayo ni makosa kwa yeyote atakayetenda dhidi ya mtoto:

- Udhalilishaji watoto kijinsia
- Utumiaji potofu wa watoto kijinsia
- Kukeketa watoto wa kike
- Kuingiza watoto katika masuala ya umalaya.
- Mwanaume kumwingilia kwa kujamiiana na mtoto aliye na umri wa chini ya miaka 18

- Mwanaume kumwingilia Kwa kujamiiana na mtoto wa kike ambae ni ndugu wa karibu, kama binti yake au mdogo wake au mjukuu wake.
- Ukatili Kwa watoto umekatazwa kisheria. Mtu aliye katika uangalizi wa mtoto akimtesa, kumtelekeza au kutomjali au akasababisha akeketwe au kutendewa maovu na akisababisha mtoto huyo kupata madhara kiafya au vinginevyo atakuwa amekosa chini ya sheria hii na akipatikana na hatia atapewa kifungo si chini ya miaka mitano na kisischozidi miaka kumi na tano au faini ya shilingi laki tatu au vyote kwa pamoja na kifungo.

- Sheria hii pia inawezesha ushahidi wa watoto kutumika mahakamani hata kama hakuna ushahidi mwingine unaounga mkono ushahidi huo.
- Sheria hii pia imeelekeza kuwa endapo mtoto anashtakiwa pamoja na mtu mzima kwa makosa ya kujamiiana, kesi dhidi ya mtoto isikilizwe faragha na ushahidi wake vile vile.

Kwa kifupi Sheria hii inawalinda watoto dhidi ya vitendo vya ubakaji, ulawiti na unyanyasaji kijinsia na utumiaji wa watoto kwenye biashara ya ukahaba. Pamekuwepo na ongezeko kubwa la watoto wanaobakwa, kulawitiwa na kuambukizwa Virusi vya UKIMWI. Wazazi huchangia kwa kiasi kikubwa kutofungua kesi mahakamani ili haki itendeke kwa watoto hao. Wazazi huamua kukaa na mtuhumiwa kuyazungumza na kumaliza bila ya kuchukua hatua za kisheria.

**Swali**

Taja mila zinazomkosesha mtoto haki yake na ambazo hazikutajwa katika sheria ya Makosa ya Kujamiiana.

### Sheria ya Kuasili Watoto

Sheria hii inaruhusu mtu kumchukua mtoto ambaye si wake na kumfanya mtoto wake kisheria. Mtoto huyu anapochukuliwa na mzazi huyu wa aliyemuasili, anapata hadhi na haki sawa na mtoto aliyezaliwa na wazazi hawa kama vile haki ya kutunzwa, kuelimishwa hata kurithi mali ya wazazi hao.

Mtu ataruhusiwa kuasili mtoto iwapo atathibitisha kuwa anao uwezo wa kumtunza mtoto huyo kama inavyostahili. Mwanaume asiye na mke haruhusiwi kuasili mtoto wa kike.

### Angalizo Muhimu

Baada ya kuangalia sheria hizi za kulinda haki za mtoto ni muhimu kuona iwapo zinatekelezwa kama zilivyo.

Kwa kuwa utekelezaji unaweza kutofautiana mahali na mahali ni muhimu baada ya somo kujadili jinsi haki hizi zinavyotekelezwa katika sehemu mnayoishi au mnayoifahamu. Pia zipo mila na desturi nyingi zinazomkosesha mtoto haki zake.Hizi ni tofauti kila mahali.Hivyo ni muhimu zijadiliwe mila za sehemu mliyopo kuona ni zipi hazimpi mtoto haki na njia zipi zitumike ili mtoto apate haki zake.

### Wajibu wa kumpatia Mtoto Haki

#### (a) Wazazi/walezi

Mtu wa kwanza kumpa mtoto haki zake ni mzazi au mlezi wake. Mzazi hupanga au husababisha mtoto azaliwe. Hivyo haki ya mtoto ya kuishi iko mikononi mwa wazazi au walezi. Ni vizuri na sahihi mzazi kupata idadi ya watoto atakaomudu kuwatunza kulingana na uwezo wake. Ni kosa kupata watoto kisha ushindwe kuwapatia mahitaji yao muhimu pamoja na elimu. Haki ya mtoto kuishi na wazazi iko mikononi mwa wazazi. Wazazi wakitengana au

kuachana wanamkosesha mtoto haki ya kuishi na wazazi wake wote. Mtu akiamua kupata mtoto nje ya ndoa pia anamkosesha mtoto haki ya kuishi na wazazi wake wote iwapo wazazi hawa hawataishi pamoja.

**(b) Serikali**

Serikali nayo ina wajibu wa kumpatia mtoto haki. Serikali kwa kutunga sheria za kulinda haki za mtoto inatimiza wajibu huo. Pia inawajibika kuhakikisha kuwa sheria hizo zinafanya kazi kama zilivyokusudiwa. Mfano, haki ya elimu, inabidi Serikali ihakikishe kuwa kuna shule, walimu, vifaa na mtaala wa kufaa kumwelimisha mtoto. Pia ihakikishe kuwa watoto wanaelimika kutokana na elimu iliyokusudiwa. Pia serikali iwachukulie wazazi au walezi hatua za kisheria wanapokiuka wajibu na iwapatie wazazi hao nyenzo za kutimiza wajibu wao. Serikali ina wajibu wa kuyapa masuala ya watoto kipaumbele. Bajeti za elimu, afya, maji safi n.k zikuzwe badala ya kudidimizwa.

**(c) Jamii**

Jamii inayomzunguka mtoto nayo inawajibika kumpatia mtoto haki nyingine zinazotokana na jamii. Mfano, jamii inaweza kumsuta au kumkosoa mzazi anayezembea wajibu wa kulea watoto kwa ulevi au tabia ya uvivu. Jamii inaweza kuwasaidia wazazi kuhakikisha mtoto mtoro anahudhuria shule. Jamii isikubali kuona mtoto anaonewa au kunyanyaswa n.k.

***Unaweza kuorodhesha njia nyingine jamii inavyoweza kumpatia mtoto haki zake.***

**HITIMISHO**

Katika somo hili la haki za mtoto tumejadili mtoto ni nani kisheria. Nadhani umegundua tofauti ya maana ya mtoto Kama ulivyokuwa unafahamu au inavyofahamika kwa

kawaida na maana ya mtoto kisheria. Pia tumeona hadhi ya mtoto ilivyo kisheria-kuwa mtoto anapata hadhi kulingana na hali ya ndoa ya wazazi wake. Baada ya kuona maana na hadhi tuliangalia jinsi jumuiya ya kimataifa ilivyompatia mtoto haki zake kupitia Mikataba ya kimataifa ya haki za Mtoto. Mikataba hii tumeona imegusa watoto wa aina zote na haki karibu zote wanazoweza kupewa watoto. Hatimaye tumeona jinsi Tanzania inavyojaribu kulinda haki za mtoto. Lengo la kujifunza somo hili ni kuzifahamu haki za mtoto na kuona iwapo zinatekelezwa katika jamii tunayoishi. Vile vile inafaa kufikiria njia za kufanya ili watoto wote wapate haki zao. hii ni changamoto kwa yeyote atakayetumia kiongozi hiki kubuni mbinu za kueneza elimu ya haki za mtoto na jinsi ya kuweza kumpatia mtoto haki hizo.

**Maswali**

1. Pendekeza njia tatu zinazoweza kusaidia katika kuhakikisha mtoto anapata haki ya kupatiwa matunzo muhimu.

2. Serikali ifanye nini kuondoa tatizo la watoto wa mitaani na watoto wanaozaliwa nje ya ndoa?

3. Jamii na serikali ifanye mbinu gani kukomesha ajira za watoto hasa katika sehemu za migodini, viwandani n.k?

4. Tatizo la mimba za utotoni likabiliwe vipi?

# SURA YA TANO

# SHERIA ZA MIRATHI

## UTANGULIZI

Tanzania ni nchi inayotambua kuwepo kwa taratibu tofauti za ugawaji wa mirathi kwa kuzingatia tofauti ya maisha ya watu wanayoishi, mila, desturi na dini wanazoabudu. Kwa ujumla Tanzania ina aina tatu za sheria za mirathi ambazo ni;

1. Sheria za Kimila.
2. Sheria ya Kiislamu.
3. Sheria ya Kiserikali.

Uzoefu umeonesha kuwepo kwa matatizo mengi katika familia au koo pale mtu anapofariki. Matatizo hayo hutokana na maswali ya msingi ambayo yatajibiwa katika sura hii. Maswali hayo ni kama yafuatayo;

i. Nani mwenye haki ya kusimamia mirathi ya marehemu?
ii. Warithi halali wa mali za marehemu ni akina nani?
iii. Je, Mjane aliyeachwa ana haki ya kurithi au kupata chochote katika mirathi hiyo?
iv. Nini wajibu wa msimamizi wa mirathi katika kusimamia mali za Marehemu?
v. Je, wosia ni nini?

Pamoja na kuwepo kwa sheria za Mirathi kama zilivyo tajwa hapo juu, bado tunaamini nchi yoyote pia husimamiwa na kuongozwa na katiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara) inatambua na kuhimiza kuwepo kwa haki sawa baina ya wanawake na wanaume. Katiba inafafanua kuwa kila mtu ana haki ya kulindwa na kuheshimiwa utu wake wakiwemo wanawake.

Hata hivyo, mbali na kuwepo kwa utawala wa sheria na katiba, bado kundi la wanawake hasa wajane haki zao zimekuwa zikikiukwa. Wajane wengi bado wananyimwa haki ya kurithi

mali za waume zao, wanafukuzwa katika nyumba za ndoa au familia pale tu wanapofiwa, wananyang'anywa watoto na wakati mwingine hulazimishwa kurithiwa na ndugu wa marehemu. Vitendo hivi pamoja na vingine vinavyofanana na hivi vimewafanya wajane wengi kuishi maisha magumu na yasiyokuwa na uhakika.

Kama ilivyoonyeshwa hapo juu, mambo yanayohusu mirathi hayapo katika sheria moja, ingawa hiyo ni sheria nyeti na ina mguso mkubwa katika jamii. Hali hii inasababisha utata mkubwa katika kuchagua sheria ipi itumike. Hivyo basi, sura hii itaonesha mifano halisi ya kesi na jinsi mwanamke anavyonyimwa haki katika sheria hizi na hasa Sheria ya Mirathi ya Kimila.

Sura hii pia itajadili maana ya wosia, namna ya kuandika wosia, pamoja na taratibu za kufungua mirathi, wosia ukiwepo au usipokuwepo. Hii ni changamoto kwa wasomaji wetu ili wazielewe vizuri sheria hizi na kuchambua upungufu uliopo. Hii itatusaidia katika kuhamasisha wabunge wetu pamoja na serikali kwa ujumla ili hatimaye sheria hizi ziweze kubadilishwa.

## SEHEMU YA KWANZA

**Sheria zinazotumika katika masuala ya Mirathi Tanzania** Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya utangulizi, sheria za mirathi zitumikazo Tanzania zimegawanyika katika sehemu kuu tatu:-

1. Sheria za Kimila
2. Sheria za kidini kama sheria ya Kiislamu.
3. Sheria ya Kiserikali iitwayo "Indian Succession Act" iliyopitishwa huko India mwaka 1865.

Kabla ya kuzifafanua sheria hizi ni vema kuelewa maneno

muhimu yafuatayo ili kurahisisha usomaji wa sura hii. Maneno hayo ni desturi na mila.

**Desturi ni nini?**

Desturi ni tabia ya kikundi au kabila inayofuatwa, kukubalika na kutambulika katika jamii kwa muda mrefu, ambayo baadaye mtu akiivunja anakuwa amekiuka maadili ya jamii ile.

**Mila ni nini?**

Mila ni desturi zilizoshamiri (au zilizotumika kwa muda mrefu) na kukubalika katika jamii ambazo zikipata nguvu ya sheria huitwa sheria za kimila.

Ni MUHIMU kutambua kwamba MILA hubadilika kulingana na wakati na hali ya maisha ya watu (namna watu wanavyoishi).

**Swali**

Je, Katika jamii unayoishi mila zipi zimebadilika?

**Namna sheria hizi zinavyotumika;**

**Sheria za Kimila**

Watumiaji wa Sheria za Kimila ni Watanzania wote wazawa, wasio na asili ya Kiasia, Kizungu au Kisomali.

Hata hivyo, endapo itadhihirika kuwa mzawa huyu aliacha kabisa mila na desturi za kabila lake, mahakama inaweza kutumia Sheria ya Kiserikali au Sheria ya Kiislamu kama marehemu alikuwa Muislamu katika kushughulikia mirathi yake.

Sheria za Kimila zimegawanyika katika sehemu mbili:-

1. **Mkondo wa Baba**

   Makabila ambayo hurithi kufuata mkondo wa baba.

   Sheria za Mirathi za kimila tulizonazo hapa Tanzania na ambazo tayari zimewekwa katika

maandishi ni sheria za mila zilizokusanywa toka kwenye makabila yanayorithi kufuata ukoo upande wa baba. Sheria hizi zimo katika **Kanuni za Urithi TANGAZO LA SERIKALI NAMBA 358/ 1963**

Sheria hizo hutumika kwa mzawa iwapo:-

(i) Ni mwenyeji wa sehemu hiyo .

(ii) Mila hiyo iwe inatumika katika jumuiya hiyo na siyo mila ambayo imeachwa (yaani muda mrefu haitumiki).

2. **Mkondo wa Mama (Matrilineal)**

Hizi ni sheria za kimila ambazo zinayahusu makabila ambayo hurithi kupitia upande au ukoo wa mama. Kwa bahati mbaya sheria hizo za kimila hazijawekwa katika maandishi kama ilivyo kwa zile sheria za urithi kupitia ukoo wa baba. Hivyo katika mjadala wetu tutaongelea zaidi sheria ambazo ziko katika Tangazo la Serikali Na. 358/ 1963.

**Urithi katika Sheria za Kimila**

Katika sheria za kimila, kama marehemu ameacha watoto, huwa ndio warithi wakuu wa mali za marehemu. Urithi katika sheria hizi umegawanywa katika madaraja matatu.

**Daraja la Kwanza**

Mrithi wa kwanza ni mtoto wa kiume wa kwanza wa ndoa. Kama marehemu alikuwa na ndoa ya wake wengi, daraja la kwanza ni mtoto wa mke mkubwa wa ndoa. Huyu hurithi sehemu kubwa kuliko warithi wote.

**Daraja la Pili**

Daraja hili linajumuisha watoto wote wa kiume

waliosalia, ambao hurithi sehemu kubwa kuliko watoto wa kike ambao ni daraja la tatu.

**Daraja la Tatu**

Daraja la tatu ni watoto wote wa kike bila kujali umri wao au nafasi yao ya kuzaliwa. Hawa hupata sehemu ndogo kuliko wote.

Kama hakuna watoto wa kiume, watoto wa kike hupewa urithi zaidi.

Katika kanuni hizo imewekwa bayana kwamba watoto wa kike hawaruhusiwi kurithi ardhi ya ukoo wala kuiuza bali wanaruhusiwa kuitumia tu mpaka watakapoolewa au kufa.

Pamoja na kanuni hii, Mahakama Kuu ya Tanzania (Mwanza) 1989, katika kesi ya **Bernado Ephraim dhidi ya Holaria Pastory** ilitamka kuwa sheria hiyo inayobagua watoto wa kike kurithi ardhi ya ukoo ni batili.

**Watoto waliozaliwa nje ya Ndoa**

Watoto waliozaliwa nje ya ndoa hawaruhusiwi kurithi, wanaweza kurithi tu kama wamehalalishwa kwa kufuata desturi au taratibu zinazojulikana na kutambulika katika jamii hiyo.

**Mjane**

Mjane hakutajwa katika madaraja ya urithi (ingawa ni wazi kwamba mke ndiye mvuja jasho zaidi katika familia). Kwa mujibu wa sheria hiyo ya kimila, mjane inabidi aishi kwa kutegemea watoto wake ambao watarithi mali ya mume wake.

**Je, kama mjane hakuwa na watoto?**

Iwapo marehemu hakuacha watoto wala wajukuu, kaka na dada zake waliochangia baba na mama ndio warithi. Kaka wa kwanza atakuwa ni daraja la kwanza ambaye

atapata sehemu kubwa. Kaka waliobaki watakuwa daraja la pili ambao watapata sehemu kubwa kuliko daraja la tatu, na dada wote watakuwa katika daraja la tatu. Ikiwa marehemu hakuacha kaka wala dada, basi mali hiyo yaweza kurithiwa na watoto wa kaka au dada zake kama wapo. Kama wote hawapo, baba wa marehemu anaweza akarithi. Na iwapo baba hayupo, baba wadogo watarithi na kama hawapo shangazi atarithi, kama naye hayupo ndugu wengine watarithi. Kazi za warithi siku zote inasemekana ni kutunza mjane/wajane na kuwagawia asilimia kidogo sana ya mali inayoondosheka.



HATA HIVYO katika jamii yetu hili halitendeki. Mjane hatunzwi bali hudhulumiwa hata hicho kidogo ambacho sheria hiyo inasema agawiwe.

**Mjane Mgumba**

Kama mjane ni mgumba**, Sheria ya Hali ya Watu** inasema mali ya marehemu itagawanywa nusu na mjane hupewa 1/20 ya nusu ya mali ya marehemu. Pia ana haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa hadi atakapoolewa au kufariki.

**Mjane anarithi ardhi?**

Kama ilivyo kwa watoto wa kike, mjane harithi ardhi ya ukoo ila hutumia tu mpaka afe au aolewe tena. Anapaswa kutunzwa na watoto wake au kurithiwa kwa kuolewa na mmoja wa ndugu wa marehemu (kama atapenda). Hata hivyo, mjane kuolewa tena katika ukoo huo haimhalalishi yeye kurithi ardhi ya ukoo.



Wanawake hawarithi ardhi ya ukoo ila huruhusiwa kuitumia.

Hata hivyo mjane ana haki ya kuishi mahali popote anapotaka na anapaswa kupewa sehemu ya mali kidogo ya vitu vinavyoondosheka.

**Maoni**

Mila ya kurithiwa kwa kuolewa na mmoja wa ndugu za marehemu NI MILA POTOFU, MBAYA NA IMEPITWA NA WAKATI inafaa iachwe hasa ukizingatia magonjwa yaliyoko sasa hivi kama UKIMWI.

Sasa hivi ni zaidi ya miaka 45 tangu sheria hii ilipopitishwa. Tanzania sasa ina katiba ambayo lengo lake ni kuwa na taifa lenye amani na usawa kwa wote. Taifa lenye watu walio na uhuru kamili, haki na undugu wa dhati. Ili kuondoa kila aina ya ubaguzi, unyonyaji, upendeleo, unyanyasaji, na ukandamizaji, Katiba imetamka wazi KWAMBA, binadamu wote ni sawa mbele ya uso wa sheria na wana HAKI sawa bila ya ubaguzi wa aina yoyote, kulindwa na kupewa haki sawa.



Kwa maana hiyo, ni kinyume cha sheria kutunga sheria

yoyote hapa Tanzania ambayo itakuwa na aina yoyote ya ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia, rangi, utaifa, kabila, dini n.k.

**Sheria ya Kiislamu**

Ni vema kutoa ufafanuzi kwamba, Watanzania wote ambao itadhihirika kuwa wameacha mila na desturi zao na ambao Uislamu huwaongoza katika vipengele vyote vya maisha yao, pamoja na watu wengine ambao si wazawa lakini ni Waislamu hupaswa kutumia sheria ya **kiislamu katika mirathi yao.**

**Mgawo wa urithi katika Sheria ya Kiislamu**

Mjane/wajane kama kuna watoto anarithi moja ya nane (1/8) ya mali ya marehemu.

Mjane/Wajane kama hakuna watoto anarithi robo (1/4) ya mali.



Wazazi wa marehemu hupewa 1/6 ya salio baada ya kuondoa fungu la mjane/wajane.

Katika sheria ya Kiislamu, marehemu anaruhusiwa kuacha wosia kwa theluthi moja tu (1/3) ya mali yake kwa amtakaye. Theluthi mbili (2/3) ya mali yake lazima ifuate utaratibu wa Sheria za Kiislamu yaani irithiwe na warithi wake.

**Sheria ya Kiserikali (Indian Succession Act 1865)**

Sheria hii ilitungwa huko India mwaka 1865 na ikahalalishwa kutumika hapa Tanzania toka enzi ya utawala wa Waingereza.

Sheria ya Kiserikali hutumika kwa Watanzania walioacha mila na desturi pamoja na watu wengine ambao si wazawa.

**Mgawo wa urithi katika Sheria ya Kiserikali**

Iwapo marehemu ameacha watoto; 1/3 ya mali hurithiwa na mjane/wajane, 2/3 hugawiwa sawa sawa kwa watoto wote.

**Kama hakuna watoto mali hugawiwa ifuatavyo;**

- ½ hupata mjane/mgane
- ½ hupata wazazi wa marehemu au ndugu wa marehemu iwapo wazazi hawapo

**Ni muhimu kuelewa kwamba;**

Sio rahisi kuihakikishia Mahakama kuwa marehemu aliacha mila na desturi za kabila lake, hasa kama aliishi vijijini. Hivyo mara nyingi zaidi Sheria ya Kimila hutumika kugawa mirathi ya marehemu mzawa.

**Kumbuka**

Kama kuna wosia, mali hurithiwa kwa kuzingatia maelekezo ya wosia.

**Kesi za Mirathi zifunguliwe wapi?**

Ni vizuri sana kuelewa suala hili.

Kesi zinazohusu kugawa mali ya marehemu kwa Sheria za Kimila, na ya Kiislam, lazima zifunguliwe Mahakama za Mwanzo na sio Mahakama nyingine zozote. Mahakama za Wilaya/Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu hushughulikia tu mirathi ya marehemu pale ambapo Sheria ya Kiserikali hutumika. (Angalia: **Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Sura ya 11 (**Kama sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002**) kifungu cha 18(1) na 63 (ii).**

**Je, Mjane anaweza kuchagua Sheria?**

Hili pia ni suala nyeti la kutilia mkazo. Kwa kawaida, sheria zinazotumika kugawa mali za marehemu zimeshapangwa na sheria. Sheria ya Kimila kwa wazawa, Sheria ya Kiislamu kwa waislamu n.k. Hata hivyo, kuna wakati ambapo hutokea utata wa sheria ipi itumike hasa pale ambapo marehemu alikuwa ni mmoja wa jamii ya kabila fulani na papo hapo alikuwa ni muislamu. Pale inapotokea mgongano wa sheria hizi mbili au na sheria nyinginezo za mirathi, uchaguzi wa sheria gani itumike huzingatia mambo mawili yafuatayo:

(a) Maisha aliyokuwa akiishi marehemu.
(b) Nia ya marehemu.

Kama mjane anaona kwamba marehemu aliachana na desturi na mila zake, inabidi aithibitishie mahakama. Kama atafaulu, basi Mahakama itaamuru sheria nyingine ya mirathi dhidi ya ile sheria ya mila itumike katika mirathi hiyo. Kwa wastani wajane wachache sana wameweza kuthibitisha hivyo. Mfano hai ni wa kesi ya **Re Innocent Mbilinyi (Marehemu) 1969 H.C.D. NA 83**

Mjane ambaye alikuwa Mchaga aliyeolewa na Mngoni alifaulu kuithibitishia Mahakama kwamba walifunga ndoa yao ya Kikristo na walikuwa wanaishi Dar es Salaam. Marehemu aliondoka Songea akiwa na miaka kama saba hivi, na alisoma na kupata shahada yake ya kwanza. Mara chache sana walitembelea Songea au Moshi. Hivyo, waliachana na mila na tamaduni za makabila yao. Katika kesi hii, mjane alifaulu kuithibitishia mahakama kuwa sheria iliyopaswa kutumika katika mirathi hiyo ni Sheria ya Kiserikali na siyo Sheria za Kimila.

Imekuwa ni vigumu kwa watu wanaoishi vijijini kuthibitisha kuwa marehemu aliacha mila zake hali alikuwa akiishi kijijini na kushirikiana na wanakijiji katika shughuli mbalimbali za mila zao hata kama yeye mwenyewe haamini na hafuati.

**Swali**

Je Sheria za Kimila za Mirathi zinalingana na hali halisi ya maisha ya sasa? Toa maoni yako.

**Mifano ya Maamuzi ya Kesi**

Mahakimu na majaji wanasema kwamba, ikiwa sheria hii ya kimila inambagua mwanamke, wananchi wenyewe wanapaswa kupinga na kusema kwamba ni mbaya na haifai kwa kizazi hiki na kijacho. WANASISITIZA kuwa, sio mtu binafsi au kikundi cha watu wachache ndiyo wafanye hivyo bali jumuiya nzima iipinge sheria hii na wawasukume wabunge wao walifikishe suala hili bungeni ili sheria hii ibadilishwe. (Hii imenukuliwa kutoka kwenye

**Kesi ya Marko Kajubi dhidi ya Kualanima Kabali EACA 34-39.**

Katika kesi ya **Bi Verdiana Kyabuje na wengine dhidi ya Gregory Kyabuje,** Jaji Hamlyn alisema kwamba, ingawa Mahakama inakubaliana na upande wa mrufani kwamba kutofautisha wanawake na wanaume ni ubaguzi na inamnyanyasa mwanamke, Mahakama haina nguvu kupinga Sheria za Kimila. Mila hizi zinapaswa kubadilishwa na wananchi wenyewe.

**Kesi ya Felista Ishekanyoro dhidi ya Martin Banyika 1968 H.C.D. 112** pia inazungumzia mirathi.

**Maelezo**: Felista alikuwa mke wa Banyika, Martin alikuwa mtoto wa Banyika kwa mke mwingine ambao walikuwa wameachana naye

kabla ya kumuoa Felista mwaka 1954.

Banyika alifariki mwaka 1963 miaka tisa baada ya ndoa yao na Felista. Baada ya miezi sita Felista alifukuzwa kwenye nyumba na shamba.

**Hukumu**

Mheshimiwa Jaji Seaton alitoa uamuzi kwamba "katika aya ya 77 ya Sheria ya Hali ya Watu, mjane hana sehemu yoyote ya urithi kwa mali alizoacha marehemu mumewe ila anaweza akapata sehemu ndogo ya mali inayoondosheka na kutumia shamba mpaka aolewe au afe na kupata sehemu ya mazao anayolima".

**Kesi zinazoamuriwa kwa kufuata katiba**

Katiba ya Nchi inasema kwamba, binadamu wote ni sawa. Kwa hiyo majaji wengine wamejaribu kupinga sheria za ubaguzi za mirathi kwa kutumia Katiba ya Nchi. Wameweza kufafanua na kupambanua mambo kwa kina na kwa undani na kutoa hukumu zinazolenga kwenye usawa wa binadamu.

Kwa mfano katika kesi ya **Abdallah Salim dhidi ya Ramadhani (1968) H.C.D 129** Mheshimiwa aliyekuwa Jaji Mkuu Georges alitamka kwamba:- Mahakama haikusudii kuingilia mila za kabila lolote hapa Tanzania, isipokuwa madhumuni yake ni kuhakikisha mila hazitumiki kumbagua mtu yeyote.



**Maswali ya kujadili katika vikundi**

1. Unapofiwa na mume au mke ni mambo gani muhimu ambayo ungependa ufanyiwe/usifanyiwe au asifanyiwe mjane uliyemuacha?

2. Sheria za kimila za mirathi katika sehemu unayotoka ni zipi? Je unakubaliana nazo? Zipi za kuendeleza na zipi za kuacha.

## SEHEMU YA PILI

### Wosia

### DOKEZO

Unapoziangalia sheria za mirathi za nchi hii utaona kuwa upo umuhimu wa jamii kujenga tabia ya kuandika wosia. Katika sheria ya mirathi inayotumika sana kwa wananchi wengi (Sheria ya mirathi ya kimila) kuna ubaguzi wa wazi wazi dhidi ya wanawake na watoto wa kike.

Si kweli kuwa mwanaume aliyechuma mali na mke wake angefurahi kuona kuwa mke wake anaambulia patupu au hata kufukuzwa katika nyumba waliyokuwa wanaishi wote au waliyojenga kwa pamoja baada ya mume kufariki. Wanaume wengi walishituka walipoelewa kuwa hali ya sheria ilivyo inaweza kutokea kwa wake zao na watoto kupata taabu baada ya kifo chao. Pamoja na mwito wa kubadili sheria suluhisho la mara moja ni kuandika wosia ambao utatambuliwa na kukubalika kisheria. Kwa kuandika wosia mtu ana uhuru wa kuwosia mali yake kwa wale ambao ni muhimu kwake ambao mara zote itakuwa ni familia yake.

### Wosia ni nini?

Wosia ni maelekezo ya mdomo au maandishi anayotoa mtu akiagiza pindi atakapokufa mali alizoacha zirithiwe na nani.

Sheria za mirathi hutaja mambo muhimu ya kufuata katika kuandika wosia. Zipo taratibu za kuandika wosia katika kila sheria ya mirathi.

**(a) Wosia katika Sheria za Kimila**

Sheria za Wosia zimo katika jedwali la 3 la sheria iitwayo "The Local Customary Law" (Declaration) Namba 358/1963 Sheria hii inaeleza kuwa wosia maana yake ni kauli inayotolewa na mtu wakati wa uhai wake kwa hiari yake kuonesha nia yake jinsi gani angependa mali yake igawanywe baada ya kufa kwake.

Wosia upo wa aina mbili. Wosia wa mdomo na wosia wa maandishi. Kwa aina yoyote ya wosia, anayeweza kuandika au kusema ni mtu mzima mwenye umri usiopungua miaka 18 na mwenye akili timamu. Wosia lazima uwe na mashahidi ambao huchaguliwa na mwenye kutoa wosia.

Mashahidi wote wanatakiwa washuhudie kwa wakati mmoja. Warithi hawapaswi kuwa mashahidi, iwapo wamekuwa mashahidi wosia huo utakuwa ni batili, yaani utakosa nguvu za kisheria. Wosia ni siri itakayofichuliwa mwosia anapofariki.

**Wosia wa Mdomo**

Wosia huu unapaswa kushuhudiwa na mashahidi wasiopungua wanne. Watu wawili kati ya mashahidi hao wawe ni wa ukoo wa huyo mwosia; na wawili wanaweza kuwa watu baki nje ya ukoo wa mwosia. Wosia huo waweza kufutwa kwa kutoa wosia mwingine wa mdomo au kwa kutoa wosia wa maandishi. Mtu asiyejua kusoma na kuandika ndiye anayeweza kutoa wosia wa mdomo na akipenda kuandikiwa vile vile inaruhusiwa.

**Wosia wa Maandishi**

Kwa mwosia anayejua kusoma na kuandika ni vema wosia wake ukawa katika maandishi. Wosia huu unatakiwa uandikwe kwa kalamu ya wino au kalamu isiyofutika au upigwe chapa.

Tarehe ya wosia ni muhimu hivyo iandikwe. Katika wosia wanahitajika mashahidi wawili.

Mwandishi wa wosia (mwosia) aweke saini katika wosia. Kama mwosia hajui kusoma na kuandika aweke alama ya kidole gumba cha mkono wa kulia. Mashahidi washudie saini au alama ya mwosia na wenyewe waweke saini zao kwenye wosia. Mwosia atataja mtu au watu ambao anapenda wasimamie ugawaji wa mali baada ya kifo chake.(Msimamizi/Wasimamizi wa mirathi).

**Mambo ya kuzingatia**

Mwenye kuacha wosia anategemewa kuwapa urithi warithi wake wa halali na wengine anaowapenda mwenyewe.

1. Mwosia anaweza kumnyima urithi, mrithi halali iwapo tu mrithi, amemkosea mambo mazito kama:

    (a) Mrithi amezini na mke wa mwosia.

    (b) Mrithi amejaribu kumuua, kumshambulia au kumdhuru vibaya mwosia (au kumtendea mama wa mwosia mambo haya yaliyotajwa).

    (c) Mrithi bila sababu ya msingi, hakumtunza mwosia wakati wa shida, njaa au maradhi.

2. Mtu anaweza kumrithisha rafiki yake vitu au mali zake alizokuwa akizitumia mwenyewe au sehemu ya

mali yake. Lakini fungu la rafiki lisizidi la kila mrithi halisi.

**Wosia katika Sheria za Kiserikali**

Hakuna tofauti kubwa na wosia katika Sheria za Kimila bali wosia huu unatarajiwa uwe katika maandishi. Hivyo vipengele vyote vya wosia wa maandishi vinatumika. Mwosia anaweza kufuta au kuongeza maneno mengine kwa kuandika maandishi mengine ambayo itabidi yazingatie masharti ya uandikaji wa wosia.

**Wosia katika Sheria ya Kiislamu**

Kwa mujibu wa Sheria ya Kiislamu, mwosia haruhusiwi kuusia mali yake yote. Huruhusiwa kuusia 1/3 tu ya mali yake. Sehemu 2/3 ni lazima ifuate taratibu za kiislamu za ugawaji mali ya urithi.

**Mahali pa kuhifadhi wosia**

Wosia unaweza kuhifadhiwa sehemu yoyote yenye usalama kuepusha uwezekano wa kufanyiwa mabadiliko na mtu asiye mwosia. Hivyo, wosia waweza kutunzwa mahakamani, msikitini, kanisani, kwa mwanasheria n.k.

Kwa hali yoyote ile, ni muhimu mtu mzima aliyefanikiwa kuwa na mali kuandika wosia. Umefika wakati wa kuondokana na fikra potofu kuwa, mtu akiandika wosia anajichuria kufa. Vifo vipo na sasa hivi hali ni mbaya sana kwani watu wengi wanakufa kwa ajali, magonjwa kama shinikizo la damu, UKIMWI, uti wa mgongo na kadhalika.

Tabia ya kuandika wosia ni muhimu kwa mtu anayejali familia yake ambayo anaweza kuacha wosia unaotambulika kisheria.

Kulingana na sheria zinazohusika. Kama wosia haukufuata taratibu zinazotakiwa, utapingwa mahakamani.

Tujenge tabia ya kuandika wosia.

**Taratibu za kufungua Mirathi**

**(i) Wosia Ukiwepo**

Mambo yafuatayo sharti yazingatiwe katika kufungua mirathi:-

1. Mtu akifa, kifo kiandikishwe kwenye ofisi ya vizazi na vifo ya Wilaya ndani ya muda wa siku 30.
2. Msimamizi akafungue mirathi mahakamani akiwa na maelezo juu ya mambo yafuatayo.

   - Hali na aina za mali za marehemu
   - Majina na anwani za wasimamizi.
   - Maskani ya marehemu (Ni Muhimu Mirathi kufunguliwa kufuatana na maskani ya marehemu)
   - Juhudi zilizofanyika kutafuta na kuthibitisha kwamba marehemu hakuacha wosia.

Viambatanisho:-
- Cheti cha kifo
- Wosia

**(ii) Kama Hakuna Wosia**

Mambo yafuatayo sharti yazingatiwe:

1. Kifo kiandikishwe kwenye ofisi ya vizazi na vifo ya Wilaya katika muda usiopungua siku 30.
2. Mkutano wa ukoo ufanyike kumchagua msimamizi.
3. Msimamizi aende kufungua mirathi Mahakamani akiwa na:

- Nakala ya uamuzi uliotokana na mkutano wa ukoo.
- Cheti cha kifo.

4. Tangazo hutolewa na Mahakama kwa muda wa siku 90 kama hakuna matatizo (pingamizi), msimamizi hukabidhiwa barua ya kuhalalisha kugawa urithi na kulipa madeni.
5. Msimamizi hugawa mali na kurejesha nakala ya mgao mahakamani ili jalada lifungwe.

**Taarifa ya mgawo wa mali za marehemu**

Msimamizi akishakamilisha shughuli za ukusanyaji na ugawaji wa mali za marehemu, atahitajika kuandaa taarifa ya mgawo wa mali hizo. Taarifa hiyo itaonesha:

- Jina la mali (inayohamishika, isiyohamishika, pesa katika akaunti n.k).
- Namna mali hizo zilivyogawanywa kwa warithi wa marehemu (yaani Mafungu waliyopewa warithi).
- Majina ya wadai na wadaiwa wa marehemu (kama wapo na endapo wameshalipwa madeni yao na kiasi cha madeni hayo)
- Gharama za mazishi.

Hatimaye, Msimamizi atapeleka mahakamani taarifa ya ugawaji wa mali ili jalada la mirathi lifungwe.

**Ni muhimu msimamizi kuhakikisha yafuatayo;**

- Gharama za mazishi ni za kuridhisha kufuatana na hali ya marehemu.
- Gharama za usimamizi ni za kuridhisha na ziwe na uthibitisho.
- Gharama za huduma alizopata marehemu za aina yoyote ziwekwe bayana.

- Madeni anayodai/kudaiwa.

**Swali**

Wosia unachukuliwaje katika sehemu unayoishi?

## HITIMISHO

Katika Sura hii tumeona aina mbalimbali za sheria za mirathi na jinsi zinavyoelezea ugawaji wa mirathi. Tumeona pia wosia ni nini, na umuhimu wa kuandika wosia. Pamoja na hayo jambo jingine lililodokezwa ni kuhusu MSIMAMIZI WA MIRATHI ambaye anapaswa kukusanya mali na kugawa kwa warithi, na siyo kuitumia yeye kwa kujinufaisha mwenyewe.

Katika sheria hizi, tumeona namna ambavyo hazitoi haki sawa kwa mwanamke na hasa sheria za kimila. Suala hili linapofika Mahakamani, kutokana na mifano hai ya kesi zilizozungumziwa, itategemea bahati ya mtu atapata Jaji yupi, kama anashikilia kuamua kesi kufuata sheria za mila za mirathi, au kutumia KATIBA, ili ilete haki kwa wote.

Hivyo ni jukumu letu wananchi, na hasa wanawake ambao wanaguswa kwa karibu na unyanyasaji/ubaguzi wa sheria hizi kuziacha na kuihamasisha jamii kuacha ili kuwe na mabadiliko. Vile vile, tuwahamasishe wabunge wetu walijadili suala hili kwa kina bungeni ili sheria zibadilishwe kuelekea kwenye mfumo wa usawa kwa wote, bila kubaguana.

## MFANO WA WOSIA

## WAWEZA KUANDIKA WOSIA WAKO KWA MFUMO HUU

1. Huu ni wosia wangu wa mwisho mimi **……………………………….** wa S. L. P …………………………………………………………………………………….
2. Kwa wosia huu nafuta wosia zote nilizowahi kuandika.
3. Namchagua ………………………………………. ambaye anaishi …………………………. wa S.L.P …………………... kuwa msimamizi wa mirathi yangu. Natumaini atafanya kazi hii kulingana na taratibu zilizopo.
4. Nitakapokufa mwili wangu uzikwe……………………………. au mahali pengine popote ambapo pataonelewa kuwa rahisi kwa mazishi yangu baada ya kukamilika kwa taratibu muhimu za mazishi kwa mujibu wa dini yangu.
5. Madeni yangu yote yatakayokuwepo wakati wa kufa kwangu pamoja na gharama za mazishi, yalipwe mara moja baada ya kifo changu

6. Mali zangu ni ……………………………………………………………………………
   (a) ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………………
   (b) Nina akaunti zifuatazo:……………………………………………………..
   ………………………………………………………………………………………
7. Mali na fedha nilizoorodhesha hapo juu zitarithiwa na warithi wangu wafuatao:
   1. Mke/Mume wangu…………………………………………………………
      Watoto……………………………………………………………………
      ………………………………………………………………………………
      ………………………………………………………………………………

i) ……………………………………………………………………………………………………

S.L.P………………………..………………… Simu:………………..………………

ii) ……………………………………………………………………………………………………

S.L.P…………………………………………… Simu:…………………..……………

iii) ……………………………………………………………………………………………………

S.L.P………………………..…………… Simu:………………………………..…………

**Imetiwa saini hapa ………………………………………………………….**

**Siku ya ………………………………………………………………………….**

**Mwezi wa …………….……………… mwaka ……………….………….**

**Saini ya Mwosia:**

Jina: …………………………………………………………………..……………………..

Saini: ……………………………………………………………………….……………..

Anwani: ………………………………………………………………………………….

Kazi: ……………………………………………….…………………………………………

**Shahidi wa Pili:**

Jina: ………………………………………………………………………………………

Saini: ………………………………………………………………………….………

Anwani: ……………………………………………………………………………..

Kazi: ……………………………………………………………………..……………………

**Mbele ya:**

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………..

**Mshuhudia viapo/saini**

…………………………………………………………………………………………………….

# SURA YA SITA

# SHERIA YA MAKOSA YA KUJAMIIINA

## UTANGULIZI

Katika muongo wa mwisho wa karne ya ishirini, jamii ya Kitanzania ilishuhudia kuporomoka kwa maadili kwa kiwango cha juu. Maeneo ambayo yalionekana waziwazi ni hili la kuongezeka kwa matukio ya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Vitendo vilivyokithiri zaidi ni vile vya dhihaka kwa wanawake juu ya maumbile yao na pia vitendo vya kuwaingilia wanawake na watoto bila ridhaa yao na kubwa zaidi ni vitendo vya kuwaingilia kinyume na maumbile.

Moja ya mambo yanayoweza kuleta mabadiliko katika mienendo ya watu ni sheria. Sheria imedhihirisha kwa kiwango fulani kuwaogofya watu kutokana na adhabu zinazotolewa baada ya mtu kuzivunja na hivyo kuwafanya kuacha au kupunguza vitendo vinavyokatazwa na sheria.
Ili kukidhi matarajio ya jamii, mwanzoni mwa mwaka 1998 serikali kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali ilipeleka muswada bungeni ili kurekebisha hali ya mmomonyoko wa maadili.

Muswada huo baadaye ulikuwa sheria inayoitwa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998 ambayo ililenga kubadili sheria mbali mbali kwa kuweka vipengele maalum katika sheria hizo kuhusiana na makosa ya kujamiiana. Sheria hii kimalengo inalenga kulinda utu, heshima, uhuru na usalama wa wanawake na watoto.

### Tafsiri ya baadhi ya Maneno ya Msingi

Ili kuondoa utata na kueleweka zaidi, sheria hii kama zilivyo sheria nyingine nyingi katika sehemu yake ya kwanza imeeleza na kutafsiri baadhi ya

maneno ambayo pengine kama yasingeweza kuelezwa (kutafsiriwa) basi yangekuwa na uwezekano mkubwa wa kutolewa tafsiri mbalimbali zenye utata na hivyo kuleta ugumu kiutekelezaji. Baadhi ya maneno yaliyotolewa tafsiri ni kama yafuatayo:-

1. ***Mtoto wa kiume*** ni mtu wa jinsi ya kiume mwenye umri chini ya miaka 18.
2. ***Mtoto wa kike*** ni mtu wa jinsi ya kike mwenye umri chini ya miaka 18.
3. ***Mwanamke*** ni mtu yeyote wa jinsi ya kike mwenye umri wa zaidi ya miaka 18.
4. ***Kutengana*** kunajumuisha kutengana kwa mke na mume kulikotokana na utaratibu wa kifamilia au kulikotokana na maamuzi ya wakubwa wa ukoo hata bila wahusika kwenda mahakamani au vinginevyo.
5. ***Kujamiiana*** kwa minajili ya kiushahidi, ili kuthibitisha kosa la kujamiiana inahesabika tendo hilo limefanyika iwe kimaumbile au kinyume na maumbile, iwapo kuna muingiliano tu na sio mpaka kutoka kwa mbegu za kiume.

**Mabadiliko katika Sheria zinazogusa Makosa ya Kujamiiana**

Kimsingi, sheria hii ya Makosa ya Kujamiiana imefanya mabadiliko katika sheria tano ambazo zinahusiana moja kwa moja na makosa ya kujamiiana. Sheria zilizofanyiwa mabadiliko ni (i) Sheria ya Kanuni ya Adhabu (ii) Sheria ya Ushahidi ya Mwaka 1967 (iii) Sheria ya Watoto na Vijana Wadogo (iv) Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu ya Mwaka 1972 na (v) Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai ya Mwaka 1985.

**Sheria ya Ushahidi ya Mwaka 1967 (Sura ya 6 ya Sheria za Tanzania kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002**

Katika Sheria ya Ushahidi ya mwaka 1967 mabadiliko yake ni yale ya kifungu kinachohusu namna ya kuchukua ushahidi wa mtoto na mwathirika wa makosa ya kujamiiana.

Kifungu hiki kimepunguza makali ya uchukuaji wa ushahidi wa mtoto mdogo kwenye kesi za makosa ya kujamiiana.

Chini ya mabadiliko haya mahakama baada ya kujiridhisha na ushahidi wa mtoto aliyefanyiwa kitendo cha kujamiiana inaweza kumtia mshtakiwa hatiani bila kutaka ushahidi wa ziada wa mtu mzima kuupa nguvu ushahidi huo wa mtoto.

**Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai (Sura ya 20 ya Sheria za Tanzania – kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002)**

Kesi zinazohusu makosa ya kujamiiana zitasikilizwa kwa faragha na hazitapaswa kutolewa katika vyombo vyovyote vya habari.

**Muhimu**: *Mwenendo wote wa kesi za kujamiiana chini ya sheria hii zinatakiwa kufanyika faragha. Aidha mahakama zimeongezewa mamlaka ya kuamuru fidia itolewe kwa mwathirika kulingana na kiwango cha kuathirika kwake.*

**Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu (Sura ya 90 ya Sheria za Tanzania – kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002)**

Mahakama katika kutoa adhabu kwa mkosaji wa makosa ya kujamiiana haifungwi na Sheria ya Kiwango cha Chini cha Adhabu bali huadhibu kulingana na adhabu inayotolewa katika sheria ya Makosa ya Kujamiiana.

**Sheria ya watoto na vijana wadogo (Sura ya 13 ya Sheria za Tanzania – kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002)**

Sheria ya Makosa ya Kujamiiana imetamka bayana kuwa iwapo shahidi au mshtakiwa ni mtoto mwenye umri chini ya miaka 18, basi kesi hiyo ya makosa ya kujamiiana itafanyika faragha.

**Mabadiliko katika Sheria ya Kanuni ya Adhabu (Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania – kama Sheria zilivyorekebishwa mwaka 2002)**

**Kosa La Kubaka**

Moja kati ya mabadiliko yaliyotiliwa mkazo sana katika Sheria ya Kanuni ya Adhabu ni mabadiliko juu ya kosa la kubaka. Kubaka ni kosa la jinai kwa mtu wa jinsi ya kiume kumwingilia (kujamiiana) msichana au mwanamke katika mazingira yafuatayo:

i. Sheria inamtaka kwamba mtu wa jinsi ya kiume atakuwa ametenda kosa la kubaka endapo atamwingilia (atajamiiana) msichana au mwanamke ambaye si mke wake, au kama ni mke walitengana bila ridhaa yake.

   Kimantiki sheria inazuia mwanaume kumwingilia mwanamke au msichana bila ridhaa yake hata kama ni mke wake, iwapo watakuwa wametengana.

ii. Pia kisheria, mtu wa jinsi ya kiume atahesabika amebaka endapo atajamiiana na mwanamke au msichana kwa ridhaa yake ambapo ridhaa hiyo imepatikana kwa matumizi ya nguvu/vitisho au kwa kumweka mwanamke au msichana huyo kwenye hatari (hofu) ya kifo au

kumuumiza au kama mwanamke au msichana huyo atakuwa amewekwa kwenye kizuizi kinyume cha sheria.

iii. Sheria inaainisha mazingira mengine ya kubaka kuwa ni pale ambapo mtu wa jinsi ya kiume atajamiiana na msichana au mwanamke kwa ridhaa yake ambapo ridhaa hiyo imepatikana katika wakati (muda) ambao mwanamke au msichana huyo hakuwa na akili timamu au alikuwa katika hali ya ulevi uliotokana na aina yoyote ya madawa ya kulevya au kitu chochote alichopewa na mwanaume au watu wengine. Labda ithibitishwe kwamba, kulikuwa na ridhaa kwa matendo ya kilevi. Kitafsiri, ridhaa inayozungumziwa na kukubalika kisheria ni ile aliyoitoa mwanamke au msichana akiwa na akili timamu.

iv. Mtu wa jinsi ya kiume anachukuliwa kuwa ametenda kosa la kubaka endapo atajamiiana na msichana au mwanamke kwa ridhaa yake ambapo mwanaume anajua kuwa yeye si mume wa mwanamke au msichana huyo na kwamba ridhaa imetolewa kwa sababu mwanamke amefanywa kuamini kuwa yule mwanaume ni mume wake halali kisheria.

v. Aidha sheria inamchukulia mtu yeyote wa jinsi ya kiume kuwa amebaka endapo atajamiiana kwa ridhaa au bila ridhaa na msichana wa chini ya umri wa miaka 18, vinginevyo basi huyo msichana awe ni mke wake ambaye ana miaka 15 au zaidi na wawe hawajatengana.

Katika kudhibiti makundi mbalimbali katika jamii ambayo kwa nafasi zao huweza kutumia

mwanya huo na hivyo kusababisha kutenda makosa ya kujamiiana, sheria imedhibiti matendo yao kama ifuatavyo:-

a) Mtu yeyote ambaye yuko katika nafasi ya mamlaka na akatumia nafasi hiyo ya kiofisi kujamiiana na msichana au mwanamke katika mahusiano ya kiofisi au kumzuia kinyume cha sheria ili ajamiiane naye, basi sheria inatamka bayana kuwa hiyo ni aina mojawapo ya kubaka.
b) Mtu yeyote ambaye yuko katika nafasi ya kiutawala (menejimenti) au mtumishi katika sehemu za kuhifadhia watoto wahalifu au sehemu zozote za kuhifadhi zilizoainishwa kisheria na akatumia nafasi hiyo na kujamiiana na msichana au mwanamke bila ridhaa yake. Sheria inabainisha kuwa hii pia ni aina nyingine ya mazingira ya kubaka kwa mtu aliye madarakani.
c) Mtu yeyote ambaye yuko katika nafasi ya menejimenti au mtumishi wa hospitali na akatumia nafasi yake kutenda kosa la kujamiiana hii pia kisheria ni aina mojawapo ya mazingira ya kubaka.

d) Mtu yeyote ambaye ni mganga wa kienyeji na akatumia nafasi yake na kutenda kosa la kujamiiana kwa mteja wake anayempa matibabu basi sheria inatambua mazingira hayo kama ni moja ya mazingira ambayo kosa la kubaka linaweza kutendeka.

Kwa minajili ya kuthibitisha kosa la kubaka, sheria inabainisha kuwa hata muingiliano (mpenyo) kidogo unatosha kuthibitisha tendo la kujamiiana. Aidha sheria kwa kutambua mazingira ya usiri yanayozunguka kosa la kubaka inatamka na kukubali ushahidi ambao huweza kujitokeza katika harakati za mtu kutaka

kujamiiana na mwanamke au msichana bila ridhaa yake. Kwa mfano; maumivu au kuumia kimwili unakubalika kama ni ushaidi muhimu kuthibitisha tendo la kujamiiana bila ridhaa.



**Adhabu kwa kosa la kubaka**

Adhabu kwa mtu atakayepatikana na hatia ya kosa la kubaka ni kuhukumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha maisha, la kama si hivyo endapo mahakama itaonelea vema kutoa adhabu ya kifungo pungufu, basi kifungo hicho siyo chini ya miaka 30 pamoja na viboko na faini. Juu ya adhabu hiyo mkosaji atatakiwa pia kutoa fidia kwa mtu aliyembaka (muathirika) katika kiwango kitakachoamuriwa na mahakama kulingana na athari alizopata aliyebakwa.

Katika mantiki ya kumlinda mtoto na bila kuathiri vipengile vingine vya sheria yoyote, endapo kosa la kubaka limefanywa na mtoto wa kiume mwenye umri chini ya miaka 18 basi mtoto huyo atahukumiwa kama ifuatavyo:

i. Kama ni mara ya kwanza kutenda kosa hilo atahukumiwa kuchapwa viboko peke yake bila adhabu nyingine yoyote.
ii. Kama kosa hilo ni mara ya pili kwa mtoto huyo kutenda, basi atahukumiwa kifungo cha miezi kumi na miwili jela pamoja na viboko.
iii. Na kama hiyo ni mara ya tatu kwa mtoto huyo kutenda kosa la namna

hiyo, basi atahukumiwa kifungo cha maisha.

Na kwa upande mwingine na bila kuathiri vipengele vingine vya sheria hii, yeyote atakayepatikana na hatia ya kumbaka msichana mwenye umri wa chini ya miaka kumi basi atahukumiwa kifungo cha maisha.

**Kubaka kwa kundi**

Endapo mtu zaidi ya mmoja watatenda kosa la kumbaka msichana au mwanamke, basi kitendo hicho kisheria huitwa kubaka kwa kundi (Gangrape). Kubaka kwa kundi kunajumuisha watu wote watakaotenda tendo lenyewe la kubaka au watakaosaidia kwa namna yoyote katika kutendeka kwa kosa la kubaka.

**Kujaribu kubaka**

Mtu atahesabika kuwa ametenda kosa la kujaribu kubaka endapo kwa dhamira yake atajaribu kufanya tendo la kujamiiana na msichana au mwanamke kinyume cha sheria. Dhamira ya mtu anayetuhumiwa kwa kosa la kujaribu kubaka inaweza kujitokeza katika matukio yafuatavyo:

a) Kwa kumtishia msichana au mwanamke kwa minajili ya kujamiiana naye.
b) Akiwa mtu mwenye madaraka au mamlaka kwa msichana au mwanamke huyo, kutumia vitendo vyovyote vya kumuogofya msichana au mwanamke huyo kwa minajili ya kujamiiana naye.
c) Kwa kufanya aina yoyote ya ulaghai kwa msichana au mwanamke ili kuweza kupata ridhaa ya msichana au mwanamke huyo.
d) Kwa kujifanya yeye ni mume wa msichana au mwanamke huyo na mwanamke au msichana huyo akawekwa katika nafasi (mazingira) ambayo itamfanya adhanie kuwa ni mume wake na bila

kufahamu angeweza kujamiiana naye kwa kudhani ni mume wake.

**Adhabu ya kosa la kujaribu kubaka**

Adhabu ya kosa la kujaribu kubaka inaainishwa katika mazingira tofauti kutegemea na namna kosa lenyewe linavyoweza kufanyika.

a) Endapo mtu atatenda kosa la kujaribu kubaka katika mazingira ya ulaghai au kujifanya mume kama ilivyoainisha hapo juu katika kipengele (c) na (d) basi adhabu yake ni kifungo cha maisha. Endapo kutokana na kesi mahakama itaona ni vema kutoa adhabu nyingine, basi adhabu hiyo itakuwa ni kifungo kisichopungua miaka 10.

b) Mtu yeyote atakayepatikana na hatia kwa kosa la kujaribu kubaka isipokuwa kwa mazingira ambayo yameelezwa hapo juu, basi atahukumiwa kifungo cha maisha na katika mazingira ambayo mahakama itaonelea vema kutoa adhabu nyingine basi adhabu hiyo ni kifungo kisichopungua miaka 30 na au bila viboko.

***MUHIMU***

*Mantiki iliyopo katika sehemu hii ya mwisho ni kuwa mahakama inaweza kuchagua aidha kumhukumu mkosaji kifungo pamoja na viboko au kifungo pekee bila viboko.*

**Bughudha Za Kijinsia**

